# *KUMTAZAMA YESU*

. . . kutoka kwenye Biblia ya Mungu. Nikijua hili, kwamba maneno yangu yakishindwa, Yake hayatashindwa. Kwa hiyo ninataka kusoma A—Andiko kutoka katika kitabu cha Isaya. Nami ninayo Maandiko niliyoandika hapa, na matamshi machache ambayo ningependa kutaja, upesi iwezekanavyo, halafu niingie moja kwa moja kuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa tena, usiku wa leo.

2 Ninataka kuichukua fursa hii, wakati tunapogeukia Isaya 45, ninataka kuchukua fursa hii kuwashukuru wahudumu wote walioshirikiana katika mkutano huu.

3 Ndugu Shores, rafiki yangu mpendwa sana, yeye anawakilisha Assemblies of God, hapa jijini. Ndugu Outlaw, rafiki yangu mwingine wa thamani, kutoka kwenye Jesus Name Church. Ndugu Fuller, kutoka Independence, rafiki yangu mwingine wa thamani. Sio tu watu hawa watatu, wanawakilisha makundi matatu makuu, lakini wahudumu wengine ambao nimewahudumia, wakati uliopita, wa miamsho mingine, wote walishirikiana na kuja pamoja, na watu wamejitokeza. Hakika ninatumaini, ndugu zangu, kwamba wengi wa watu wenu, waliokuwa wagonjwa na wahitaji, walipata usaidizi kwenye wakati huu. Nami nina hakika kwamba nilijaribu yote niliyojua, nami nina hakika Roho Mtakatifu atathibitisha yale yaliyokwisha kusemwa na kufanywa.

4 Kwa hiyo, Bwana awabariki sasa tunapoiangalia Biblia. Isaya 45, kuanza kwenye mla- . . . wa 22 au kifungu cha 22.

> *Niangalieni mimi, mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia; maana mimi ni Mungu; hapana mwingine.*
>
> *Kwa nafsi yangu nimeapa, neno hili limetoka kinywani mwangu katika haki, wala halitarudi, ya kwamba mbele zangu kila goti litapigwa,* na *kila ulimi* utajibu.

5 Ninajua huo sio usomaji mwingi wa Maandiko, bali huo unatosha kwani ni wa Milele. Ni Neno la Mungu. Na kama nitaliita hili fungu sasa, kwa yapata dakika ishirini, au thelathini, ningependa kusema, ninataka kusema: *Kumtazama Yesu*.

6 Huo umekuwa ndio wito kwa miaka, "Niangalieni Mimi, enyi ncha za dunia." Ningependa kwa namna fulani kugeuza hilo kidogo tu, na, "Niangalieni hasa Mimi kwenye mwisho wa kila mfumo wa ulimwenguni," kwa kuwa daima Yeye hujitambulisha dhahiri sana kwenye mwisho wa mfumo wa ulimwenguni wakati unapofikia mwisho wake. "Niangalieni Mimi, enyi ncha zote

za ulimwengu," naweza kusema. Maandiko yanasema, "Miisho, miisho ya dunia," miisho ni wingi, "miisho ya dunia."

7 Wengi husema, "Tumesikia hili kwa miaka mingi, 'Niangalieni Mimi. Niangalieni Mimi.'" Vema, hiyo ni kweli. Lakini jambo, swali ni kwamba, ni kitu gani unachoona unapotazama? Umeulizwa hilo kwa muda mrefu, "Niangalieni Mimi."

8 Unawasikia watu wakisema, "Tazama." Wakilitaja neno tazama, linamaanisha, "kuzingatia, kuangalia juu, au kutazama, na kuchunguza."

9 Na sasa Mungu anasema hapa, "Nitazameni Mimi. Mimi ni Mungu, na hapana mwingine."

10 Nami nashangaa, katika wakati tunaoishi sasa, ni kitu gani ambacho tungaliweza kuangalia kilicho halisi kuliko Mungu? Naye Mungu ni Neno, kwa hiyo liangalie Neno la Mungu, leo, kwa ajili ya jibu lako. Biblia inalo jibu kwa ajili ya siku hii. Imekuwa nalo kwa ajili ya siku zingine. Inalo milele, kwa sababu ni Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

11 Biblia inalo jibu, kwa sababu Biblia ni ufunuo wa Yesu Kristo, akifunuliwa tangu msingi wa ulimwengu. Amefunuliwa katika umbo la manabii, amefunuliwa katika umbo la wafalme, amefunuliwa katika umbo la watoa-sheria, kwa sababu hicho ndicho alicho: Mfalme, Nabii, Mtoa-Sheria, na Mungu.

Sasa, Yeye alisema, "Nitazameni Mimi."

12 Na wewe unasema, "Nimefanya hivyo." Inategemea kile ulichoangalia, inaamua kile unachoangalia, ni wapi na sababu gani ya kumwangalia. Unaangalia nini? Una kusudi gani katika kumwangalia? Inategemea tu sababu yako ya kuangalia, hiyo ndiyo unayopata.

13 Kwa kawaida, watu huja kwenye mkutano, mkutano wa kidini, baadhi yao huenda ili kupata umati mkubwa wa watu kuketi nao. Wengine . . . Loo, nachukia kusema hili, bali ni kweli. Wengine huenda kanisani ili tu kuonyesha nguo zao wanazovaa. Wengine huenda kanisani kwa sababu wanasema, "Hili ndilo kanisa kubwa kuliko yote jijini; ama lina—lina jina bora kuliko yote; tabaka fulani la watu huhudhuria kanisa hili," basi hilo ni—hilo ni kosa. Mnaona? Huangalii kitu kifaacho kilichofanya kanisa kuanzishwa.

Mungu alisema, "Niangalieni Mimi."

14 Watu wengi huenda kwenye ibada na ili tu kuonekana. Na wakati mwingine watu huenda kwenye ibada . . . Hili ni baya sana kusema jambo hili, na tungeweza kukaa kwa hilo muda mrefu. Lakini wanaenda kanisani huku wamechukua msimamo wao kabla ya kuenda. Iwapo mambo fulani yatasemwa, ama jambo fulani kinyume na wazo lao, watasimama moja kwa moja

na kuondoka. Kamwe hawatavumilia hata, kwa maana wanalo wazo lao kile halina budi kuwa.

15 Hiyo ndiyo sababu hasa kwamba Yesu hakueleweka wakati alipokuja duniani. Kama wangaliangalia tu katika Neno la Mungu, badala ya ninii yao—ya mapokeo yao ya siku zile, wangalijua kwamba alikuwa ni Mwana wa Mungu. Kwa sababu, Biblia ilitangaza wazi kuja Kwake kikamilifu, Naye alikuja katika ufunuo mkamilifu wa Neno.

16 Na kila kizazi humfunua katika ufunuo mkamilifu uliotengwa kwa ajili ya wakati huo.

17 Kizazi hiki hakina budi kumfunua Yesu Kristo. Huo ni ufunuo Wake aliyeahidiwa katika Neno, hauna budi kufunuliwa kwa kizazi hiki. Ikiwa makanisa hayataupokea Huo, mtu fulani atainuka na kuupokea.

18 Maana, Yohana alisema, "Mungu anaweza kutokana na mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Msiwazie kusema ndani yenu, 'Tunaye Ibrahimu baba yetu,' kwa kuwa Mungu anaweza kutokana na mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto."

19 "Kwa kuwa kile alichosema Mungu, Mungu anaweza kabisa kutimiza kile alichoahidi kutenda. Baba yetu Ibrahimu alitambua hilo, na kinyume na matumaini aliamini katika tumaini; wala hakusitasita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; bali alikuwa na nguvu, akimpa Mungu sifa, kwa sababu Mungu alimpa ahadi."

20 Ametufanyia ahadi kwa ajili ya siku hii. Ametufanyia ahadi. Na ahadi yetu leo ina hakika tu kufunuliwa kama ilivyokuwa kwa Ibrahimu, kwani sisi ndio watoto wa Ibrahimu, "Tukifa katika Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu, na warithi pamoja Naye kulingana na ahadi."

21 Watu wengi sana wanakuja, wameweka msimamo wao, wanaketi kwenye mkutano wa Full Gospel, ama mkutano mwingine wowote, nao watangojea tu dakika chache mpaka jambo fulani lisemwe ambalo hawakubaliani nalo, ndipo wanasimama na kuondoka. Hawatakaa kusikiliza zaidi. Wana . . . Hawatakaa kuona kama kulikuwako, na ni nini Ukweli wake.

22 Sasa tunasema, "Je, hiyo ni roho? Hiyo ilitoka wapi?" Imekuwako daima. Hiyo ilitoka Mwanzo. Ilikuwepo kote katika Maandiko. Mara nyingi . . .

23 Wakati Paulo alipokuwa akinena wakati mmoja, hasa, kwa kundi la watu, mbona, wa—walimsikiliza kwa makini mradi tu alidumu kwenye torati. Lakini alipoanza kunena kuhusu ufunuo, ono la Kimbinguni, upesi ulibadilisha kusanyiko. Walisimama, kupiga mayowe. Iwapo wangalisikiliza tu yale mtu huyo aliyosema, alikuwa akifunua Kweli ya Mungu, kwa Neno.

24 Wakati fulani uliopita, katika jiji kubwa, hapa Marekani, nilialikwa kwa uamsho. Ni watu wachache—wachache sana ndio waliohudhuria. Labda, katika mkutano wote, hakukuwa na zaidi ya waliopo papa hapa katika jengo hili usiku wa leo. Nami nikawazia, "Vema, ningetoa ki—kiamshakinywa, kiamshakinywa cha bure." Ndipo nikachukua matoleo yangu ya upendo ili kukifanya kiamshakinywa kuwa bure kwa baadhi ya waaminio wa ekumeni hapo kwenye jiji, na kuwaambia "Wajitokeze, ningetaka kuzungumza nao na kuwaambia sababu yangu ya kuwa kule: kulisaidia jiji, kuwasaidia wagonjwa, kuwasaidia, kila kanisa."

25 Vema, asubuhi hiyo, wakati Daktari Lee Vayle alikuwa mnenaji wangu kwenye uamsho, alikuwa amenitambulisha kwa wa—wasikilizaji, baada ya kiamshakinywa, ndipo nikachukua ninii—fungu hili, "Sikuliasi lile ono la Mbinguni." Katika kitambo kidogo tu, nilimwona mhudumu aliangalia saa yake, akainama na kumwashiria yule jamaa mwingine kwa kichwa, akasimama na kuondoka. Kabla sijasema maneno sita au manane, karibu theluthi moja ya kundi hilo la wahudumu walikuwa wameondoka. Kabla ya kuwa na dakika tano ya kuzungumza tu kile Paulo alichosema, kwamba yeye "hakuliasi ono la Mbinguni," kwa sababu Mungu alikuwa amemwita kwa kazi hii, waliona papo hapo ambapo nilikuwa ninaelekea kuwekea msingi wazo langu. Hakukuwepo na zaidi ya theluthi moja ya kundi hilo waliosalia. Sasa huko hata si kuchukua fikira ya Mkristo, kama mtu ambaye angeliitia Jina la Yesu Kristo.

26 Ninasema hili kwa heshima, bali ninalisema kusudi lizame. Nilikuwa na uelewano zaidi, na ushirika ulio bora zaidi, na kundi la Waafrika wachawi kuliko nilivyokuwa nao na lile kundi la wahudumu asubuhi ile. Walitoa nafasi zaidi kwa Neno la Mungu, na kuuliza maswali, kwa ajili ya . . . ili niweze kuwapa tumaini lililoko ndani yangu, kwa ajili ya tumaini la Uzima wa Milele.

27 Wahudumu hawa hawakuwa na muda kwa ajili Yake hata kidogo. Upesi tu, punde tu ungesema jambo fulani, wangeondoka moja kwa moja. Na kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo. Walikuwa wamechukua msimamo, wanakaa tu muda fulani, na hayo ndiyo yote wanayotaka kujua. Kama ni Neno moja halikubaliani na kitu chochote kidogo wanachoamini, hawawezi kukaa na kusikiliza Hayo yote. Hiyo ndiyo sababu wasingeweza kumwamini Yesu Kristo katika kuja Kwake kwa kwanza. Hiyo ndiyo sababu watamkosa katika kule kwa Pili.

28 Wanamkosa kila wakati. Daima wamemkosa. Naye amejifunua Mwenyewe katika Musa, akajifunua Mwenyewe katika Nuhu, akajifunua Mwenyewe katika Eliya, manabii wote, waliukosa kila wakati. Yesu alisema, "Ni yupi kati ya baba zenu ambaye hakuwaweka manabii katika makaburi huko

nje wanayoyapaka rangi sasa?” Hiyo ni kweli. Daima imekuwa kweli. Ni kweli hata leo hii.

29 Na, hata hivyo, miongoni mwa haya yote, tumeamriwa kutazama. “Mwangalieni Yeye, enyi ncha zote za dunia.”

30 Wakati mwingine wanaingia, mtu atakuhukumu kwa aina ya nguo. Kama hujavaa nguo za huduma, na kadhalika, basi hiyo iko nje, hawatakuwa na uhusiano wowote nawe. Wakati mwingine wanataka kuangalia kuona ni aina gani ya elimu uliyo nayo, kama unatamka maneno yako vizuri, kama unasimama sawasawa, jinsi unavyotumia nomino zako na viwakilishi nomino.

31 Kusema kweli, sijui ni gani nomino au kiwakilishi nomino. Sijui. Kwa hiyo, hiyo, hiyo iko nje, kwangu mimi, nami si—sijui kabisa. Nisingeweza kujua tofauti kati ya nomino na kiwakilishi nomino. Nilijua nilipokuwa shuleni, bali nimesahau hayo muda mrefu uliopita.

32 Ninajua tu kitu kimoja, na hicho ni Yesu Kristo katika nguvu za kufufuka Kwake, hicho ndicho chote ninachojua kusema habari zake. Viarifa na viwakilishi nomino, sijui chochote. Na ninafikiri hayo ndiyo hutuleta sote pamoja kwenye mikutano kama huu, ni kumjua Yeye; si kujua nomino na viwakilishi nomino, bali kumjua Yeye, Yesu Kristo, katika nguvu za kufufuka Kwake.

33 Sasa, watu wengine, wanapomwangalia Yesu, wanaangalia na kumwona, wanaangalia na kumwangalia Yeye, na, halafu wanamwona, wanaona katika Yeye mwanzilishi tu wa kanisa, ama m—m—mwundaji wa kanisa, ama labda ka—kanuni ya imani ya kanisa. Hicho ndicho watu wengi humwangalia Yesu kuona. Yeye ni kanuni mpya tu ya imani iliyoongezwa kwenye mafundisho ya kale. Sasa watu wengi huangalia na kumwona namna hiyo.

34 Wengine huangalia na kumwona Yeye kama hadithi ya uongo, Santa Claus. Au, baadhi yao humwangalia Yeye kama tukio fulani la kihistoria ambalo Mungu alifanya miaka mingi iliyopita. Baadhi yao humwangalia Yeye bado kama mtoto mchanga katika hori.

35 Lakini, swali ni kwamba, je! wewe unaona nini unapomwangalia? Je! unaona mtu wa pili katika utatu, ama unaona utatu, watatu ndani ya Mmoja? Utamwona Yeye tu kama unavyomwangalia kupitia Neno. Hiyo ndiyo njia pekee unayolifahamu Hilo, kwa maana Yeye ni Neno. Litamfunua Mwenyewe. Inategemea kile unachotazamia.

36 Kama ukimwangalia Yeye, ili kubishana, basi unaangalia vibaya. Yeye hakubishana. Haikumpasa Yeye kubishana.

37 Kumbukeni, unamwona Yeye jinsi unavyomwangalia kupitia Neno Lake, na kumtambua Yeye. Sasa huwezi kumwona mpaka

macho yako yafunguke kwa kweli hiyo. Watu wawili wanaweza kuliangalia Andiko moja na wasikubaliane; mmoja wao hana budi kuwa sahihi, na huyo mwingine makosani.

38 Wakati mwingine kuna mambo yanayotukia karibu na sisi, ambayo hatuwezi kuyaelewa; baadhi wanasema wanaona mambo fulani, wengine hawaoni chochote kuyahusu.

39 Angalia huko chini Dothani, siku ile wakati Eliya alipokuwa amezungukwa na jeshi la Shamu. Naye mtumishi wake mwaminifu, Gehazi, aliyeishi pamoja naye, akamtunza, akampikia, na kufua nguo zake, akamuosha mikono yake; alikuwa moja kwa moja pamoja naye, mchana na usiku, akamsikiza akifundisha na kuhubiri. Na asubuhi hiyo alipoamka, aliangalia nje na kuona jeshi la Shamu wamezunguka kote; akasema, "Baba yangu, ole! Angalia upinzani tulio nao, jeshi lote la Shamu!"

40 Mnaona, Eliya, alipoamka, na kuangalia, aliona kitu ambacho Gehazi hakuona. Na kwa hiyo akaomba, "Mungu, mfumbue macho kijana huyu." Sasa, macho yake yalikuwa yamefunguka kabisa, bali alisema, "Yafumbue macho yake, ili aweze kuona." Basi macho yake, kiroho, yalipofumbuka, milima yote ilijaa magari ya Moto na Malaika kote kumzingira nabii. Mnaona, ilikuwa tofauti macho yake yalipofumbuka.

41 Sasa, watu hutazama Neno, kikawaida, na hivyo ndivyo unavyopaswa kuliangalia, bali Hilo hujitangaza lenyewe kikawaida na kiroho pia. Roho hulifanya Neno kuitimiza ahadi. Kwa maneno mengine, Hilo ni Mbegu, Roho huipa Uhai. Hulitia nguvu, Hilo hulipa—hulipa uwezo, kama vile mvua huipa mbegu iliyozikwa ardhini. Huchipua, Uhai. Na wakati ukimwangalia Yesu kama Neno lililoahidiwa la wakati huu, basi litafunuliwa kwako. Ukimwangalia Yeye, utaona kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele, Kristo yeye yule.

42 Sehemu ya Neno la Mungu imetengwa kwa kila kizazi, kote kuanzia Mwanzo. Mungu daima humtuma mtu. Kwa kawaida utawala wa kidini huchanganya Hilo sana hata linaingia katika mapokeo, na kadhalika, kama ilivyokuwa katika kuja kwa Yesu, ndipo basi Mungu humtuma nabii. "Neno la Bwana humjia nabii," yeye hulifunua. Anapigwa mawe hata kufa, au kutengwa, kuondolewa; ndipo basi, kitambo kidogo baada ya yeye kuondoka, wanajenga kaburi lake na kusema alikuwa ni mtu mashuhuri. Wanaishi katika kivuli cha kile alichokuwa huko nyuma, na kulikataa Neno linaloendelea leo hii.

43 Ni kama tu mwanadamu: daima anazungumza kuhusu jinsi Mungu alivyo mkuu na yale aliyofanya, jinsi ambavyo mambo atakayofanya, na kutoona yale anayofanya sasa hivi. Mnaona? Anamwangalia Yeye katika historia, anamwangalia katika unabii, bali anasahau ya kwamba Yeye anafanya jambo

lile lile hivi sasa kama alivyofanya wakati ule. Hiyo iko tu katika mwanadamu, hata hivyo.

44 Tuliona wanafunzi, wakati mmoja, baada ya . . . Vema, ilikuwa ni asubuhi ya kwanza ya Pasaka. Ni asubuhi ya jinsi gani! Yesu, amefufuka kutoka kwa wafu, anatembea katikati ya maua. Nao marafiki wawili, Kleopa na mmoja wa rafiki zake, walikuwa njiani wakienda Emau. Nao walikuwa wanatembea wakizungumza, wamehuzunika moyoni mwao. Ndipo Mtu akatoka kichakani, akatembea pamoja nao siku nzima, akiwazungumzia kumhusu Kristo. Basi jioni hiyo, wakamwuliza. Alifanya kana kwamba alikuwa anaenda kupitiliza, lakini walimwomba aingie ndani. Akaingia.

45 Ndipo, alipoingia, alifanya jambo fulani pale jinsi alivyolifanya kabla ya kusulubishwa na kufufuka Kwake. Kabla hajasulubishwa, walimwona akilitenda sawa tu na alivyotenda. Wakatambua ilikuwa ni Yeye, ingawa walishakuwa pamoja na Yeye siku nzima wasitambue kwamba Yeye alikuwa ni Nani.

46 Inawezekana, leo hii, kwamba mtu mzuri, mtu mwema, atembee na Kristo, akilisoma Neno Lake, na bado asitambue ya kwamba huu ndio wakati ambapo mambo fulani ya Biblia hii hayana budi kutimia. Ndiyo saa tunayoishi, wakati umewadia ambapo mambo haya hayana budi kutendeka. Imeandikwa, na hivyo lazima itimie kwa sababu Mungu aliahidi. Naam, macho yetu hayana budi kufumbuliwa kuweza kuliona Neno. Sasa, unaweza kuliangalia Neno . . .

47 Mafarisayo walikuwa wamelielezea Neno hilo jinsi hasa Masihi alikuwa anakuja. Waliamini walikuwa sahihi. Na hapa Yeye alizaliwa na akatembea moja kwa moja miongoni mwao, nao wakamhukumu; wakati alipowaambia, “Yachunguzeni Maandiko, kwani ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi.”

“Yachunguzeni Maandiko.”

Wakasema, “Sisi ni wanafunzi wa Musa.”

48 Yeye akasema, “Kama mngalikuwa ni wanafunzi wa Musa, mngalinijua Mimi, kwa kuwa Musa aliandika kunihusu Mimi.”

49 Na Yeye alifanya hivyo. Musa alisema, “Bwana Mungu wenu atawainulia Nabii kama mimi, mtoa sheria, na kadhalika, na Nabii, na Yeye watu watamsikia.”

50 Mnaona, kama wangalijua aliyoandika Musa, wangalimjua Yeye. Walidhani walijua aliyoandika Musa, lakini, unaona, hawakuyajua. Mnaona, walipofushwa kwa kweli hiyo.

51 Kwa hiyo maneno machache tu kutoka Kwake, namna hiyo, walifanya nini? Waliinuka na kusema, “Mtu huyu ana pepo. Ati anakuja kutufundisha sisi? Kwani alitoka shule gani Yeye? Hatuna rekodi Yake. Nashangaa ni kadi ya nani ya ushirika anayobeba?” Ama, kitu kama hicho kilikuwa ndicho swali.

52 Lakini walikosa kuangalia na kuona ya kwamba Mungu yeye yule aliyeliahidi Neno alikuwa analithibitisha papo hapo kupitia Mtu huyo Yesu Kristo, kwa kuwa Yeye alikuwa ndiye Nuru ya wakati. Alikuwa ndiye Nuru ya watu kutembea ndani yake. Na, Neno la Mungu pekee hutoa Nuru. Neno la Mungu pekee hutoa Nuru.

53 Neno la Mungu hutoa mwanga wa jua. Neno la Mungu hutoa dunia. Neno la Mungu hutoa hewa. Kila kitu ni Neno la Mungu likidhihirishwa, kila kitu kilicho na uhalisia ndani yake.

54 Wakati alipokuwa hapa, Yeye alisema, "Mimi ni Mungu, na kando Yangu hakuna mwingine."

Wengine waliangalia. Hebu tuchukue baadhi walioangalia.

55 Isaya, wakati mmoja, nabii kijana...Hapa wakati uliopita huku Phoenix, nilizungumza habari zake, kwa—kwa wafanyibiashara, naamini ilikuwa hivyo. Jinsi alivyokuwa ameegemea sana kwenye bega la mfalme, Uzia, nasi tunaona kwamba Uzia alijawa kiburi na akapigwa na ukoma. Ndipo ilimbidi Isaya kuenda hekaluni na kuomba, na kusema, amkiri kuwa ni mwenye dhambi. Ndipo akaona Makerubi wakija, huku mbawa zao zimefunika nyuso zao takatifu, na miguu, na kuruka kwa mabawa, na kulia, "Mtakatifu ni Bwana Mungu." Wakati Isaya alipopata kumwona Yesu Kristo kidogo tu, hili hapa aliloona. Hakumwona mtu tu wa kawaida. Hakumwona mwanafalsafa.

56 Kama vile mengi ya makanisa yetu ya kiprotestanti leo, nafikiri ni asilimia sitini na nane au themanini na sita ya hayo, katika uchunguzi, walikana kuamini. Wanakataa kuzaliwa kibikira kwa Yesu Kristo; wahubiri wetu wa Kiprotestanti. Hiyo ni kweli. Hii ni kutokana na takwimu. Moja kwa moja, wanakataa kuzaliwa na bikira. Hawaamini kwamba ilikuwa kweli ni bikira. Kwa hiyo, basi, Isaya hakuona kitu kama hicho. Baadhi yao, walisema, "Yeye alikuwa ni Mtu mzuri." Wengine wao, kama vile baadhi ya madhehebu yetu leo, walisema, "Yeye ni mtu mzuri. Hakika, hakuna dosari katika Yeye, ila, nawaambieni, Maneno Yake hayawezi kuimarishwa wala kuaminiwa leo hii."

57 Vema, itikadi yoyote na imani yoyote iliyojengwa nje ya Neno la Mungu, achana nayo. Yesu alisema, "Neno la kila mtu litashindwa, bali Langu halitashindwa. Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe."

58 Kwa hiyo, basi, kanuni yoyote ya imani au chochote kisichojengwa juu ya hili Neno la Mungu, Neno lote la Mungu! Yesu alisema, "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno." Sio tu Neno moja *hapa* na Neno moja *pale*, na kitu kidogo hapa na pale, na kuweka Hilo pamoja; bali, "Kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu!" Mtu atachukua kila Neno la Biblia!

Kuliweka pamoja . . . Tayari liko pamoja; lisome tu na kuliamini, ulifanyie kazi, Mungu ataliheshimu.

59 Sasa tunaona kwamba, Isaya, wakati alipoangalia. Uliona nini, Isaya? Alimwona Mmoja aliyeitwa, “Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele.” Hicho ndicho alichoangalia.

60 Kama ningalimwita mtu mwingine, Danieli, wakati mmoja ulikuwa na fursa ya kumwona Yeye. Nabii mashuhuri, uliona nini? Akasema, “Niliona Jiwe, lililokatwa kutoka mlimani, bila mikono, Nalo likabingirika hata kwenye falme za duniani na kuzivunja vipandevipande, nazo zikapeperushwa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari. Na hilo Jiwe likakua likawa mlima mkubwa ulioijaza dunia.” Hilo ndilo alilosema kumhusu Yeye.

61 Hivyo basi, Yeye ataitawala dunia, siku moja. Watu wanapambana leo kwa ajili ya mtawala wa ulimwengu; kila taifa linataka lugha yao, ma—mawazo yao; kila dhehebu linataka makundi yao kuyatawala mengine. Bali kunakuja Mmoja, na huyo atakuwa Yesu Kristo. Yeye ndiye mtawala wa ulimwengu; si mwingine pungufu ya Mungu Mwenyewe.

62 Nebukadreza, siku moja, alikuwa amefanya jambo ovu, aliwatupa wana watatu waaminio kwenye tanuri la moto. Ndipo wakati alipofungua mlango kuona jinsi walivyokuwa wakiendelea mle ndani, alimwona Mtu wa nne ndani ya tanuri. Basi uliona nini ulipoangalia, ewe Nebukadreza? Akasema, “Alionekana kama Mwana wa Mungu.” Hicho ndicho alichoona wakati alipoangalia kwenye uhalifu aliokuwa amefanya, kulikuwa na Mmoja aliyeonekana kama Mwana wa Mungu.

63 Ezekieli aliangalia siku moja, akasema, “Nilimwona, pia, na Yeye alikuwa ni Gurudumu katikati ya gurudumu, likigeuka, juu hewani.” Hivyo ndivyo alivyoonekana kwa Ezekieli.

64 Yohana, aliye mkuu kuliko manabii wote, ndiye aliyemtambulisha Yesu. Yesu alisema yeye alikuwa “mkuu kuliko mtu yeyote aliyezaliwa.” Je! uliwahi kuwazia hiyo ilikuwa ni kwa sababu gani? Wengine wote walizungumza kumhusu Yeye, “Neno la Bwana humjia nabii,” hiyo ni Biblia ilisema hivyo, na katika manabii wengine wote liliwajia katika maono. Lakini wakati Neno lilipomjia Yohana, lilikuwa mwili. Yesu alikuwa ndiye Neno. Yeye ni Neno. Daima alikuwa ni Neno, lakini hapa ndipo utimilifu wa Mungu “ulifanyika mwili ukakaa katikati yetu.” Wakati Yeye alipomjia majini, yeye alikuwa ni nabii. Na Neno likifanyika mwili, halina budi kumjia nabii. Neno, popote lilipo, halina budi kumjia nabii, kwa sababu nabii ndiye ambaye Neno humjia. Naye Yohana alikuwa ndiye nabii wa siku hiyo.

65 Na wakati Neno lilipomjia, alijitokeza akaingia majini na kusema, "Nataka nibatizwe."

66 Naye Yohana akasema, "Nina haja kubatizwa na Wewe, na mbona Wewe waja kwangu?"

67 Akasema, "Kubali iwe hivyo sasa, kwa kuwa hivi inatupasa kutimiza haki yote."

68 Je! uliwahi kuwazia ni kwa nini Yohana alisema hivyo? Ni kwa nini Yohana amwambie Yesu hivyo? Kwa nini? Kwa sababu ni. . . Iliwapasa. Walikuwa . . .

69 Hapo alikuwapo na—nabii na Neno, nalo Neno lilikuwa limemjia nabii, sasa iliwapasa kwamba haki yote haina budi kutimizwa. Kulifanyika nini? Basi Yohana akambatiza Yesu. Kwa sababu, Yohana akiwa ni nabii na alijua Neno, dhabihu lazima ioshwe kabla haijatolewa, na hiyo ndiyo sababu Yohana alimbatiza Yesu.

70 Yohana aliangalia, na akaona. Alijuaje kwamba huyu alikuwa ni Yesu? Aliona hua, aliyekuwa ameambiwa na Roho wa Mungu. "Na yule utakayemwona Roho akishuka juu Yake, na kutulia, Huyo Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto."

71 Nuhu aliangalia. Tunaona hapa, kulikuwako na mtu mwingine aliyeangalia, jina lake Nuhu—Nuhu. Aliangalia akaona haki ya Mungu juu ya . . . Hukumu ya haki ya Mungu, hasa, juu ya ulimwengu mwovu wenye kukataa Neno, ilikuwa ikimwagwa. Katika ono lake, kwa vile Nuhu alikuwa nabii, Mungu alikuwa amempa ono la jinsi ya kuijenga safina, na kumwongoza jinsi ya kufanya ujenzi, jinsi ambavyo haina budi kujengwa. Katika hili, Nuhu angewezaje, isipokuwa hili ono likiwa ni Neno la Mungu, wakati akiona ghadhabu hii na kufanya njia ya maandalizi?

72 Daima, kabla ya kuja kwa hukumu, kuna maandalizi yanayofanywa. Daima ni Neno la Mungu.

73 Na wakati alipokuwa akilijenga Neno la Mungu pamoja, akishuhudia kwamba ono lake lilikuwa kweli na aliliamini, wenye kudhihaki walimdhihaki, na kadhalika. Lakini Nuhu alikuwa ameangalia mbele na kuona haki ya Mungu ilibidi kuhitaji hukumu juu ya watu, naye akajenga safina kuokoa nyumba yake mwenyewe. Wakati alipoangalia, aliiona ghadhabu ya Mungu inayokuja, ndipo akafanya maandalizi kwa ajili ya watu kuliepuka jambo hili.

74 Vivyo hivyo na Yohana Mbatizaji, alifanya maandalizi kwa ajili ya kuepuka.

75 Vivyo hivyo na Roho Mtakatifu, leo, akitangulia Kuja kwa Yesu Kristo, analijenga jengo, Mwili wa Yesu Kristo. Tumebatizwa katika Huo; si kwa kanuni ya imani, si kwa dhehebu wala kupeana mikono. Bali, "Kwa Roho wa

Mungu tunabatizwa katika Mwili wa Yesu Kristo," jengo litakalostahimili hukumu, kwa sababu umehukumiwa tayari. "Nionapo Damu, nitapita juu yako." Naam.

Nuhu, aliangalia na akaona kilichokuwa kinakuja.

76 Musa aliangalia, siku moja, aliona Nguzo ya Moto. Ikavutia usikivu wake. Mwanatheolojia huyu mashuhuri, alikuwa amekimbia na mafundisho yake yote ya theolojia, na kuelewa kwake (kupitia mama yake) kwa Neno Lenyewe. Ya jinsi ambavyo alikuwa awakomboe wana wa Israeli. Bali alipojaribu kwa njia yake, alishindwa. Na ingawa mama yake alikuwa amemweleza kabisa juu ya jambo la kufanya, na kile angefanya, na ni nini ambacho Mungu alikuwa amemwinua kwa ajili yake. Maarifa haya yote, mazuri kama yalivyo, na ni mzuri, lakini hata hivyo ilibidi yawekwe kando. Hayo yalikuwa tu ni mitambo.

77 Mitambo siyo ambayo huendesha motokaa. Ni nguvu ndizo huiendesha.

78 Mitambo haiendeshi kanisa; ni nguvu, Roho Mtakatifu ndiye huingia ndani ya Neno hili. Si seminari inayokufundisha theolojia yote na fasiri za Kiyunani. Bali ni nguvu za Roho Mtakatifu mle ndani, kulitia Hilo moto na kulifanya litimie, na kulifanya liishi kile hasa Neno la ahadi lilicho kwa ajili ya wakati huu. Si mitambo; nguvu! Inahitaji mitambo na nguvu tendaji, Neno na Roho, hizo Ndizo hutoa Uzima.

79 Kile ambacho Mungu aliahidi kwa ajili ya wakati huu, litazamie kutimia. Huna budi kumwangalia Yeye, kwa sababu Yeye ni Neno. Na njia ya pekee ya kuliangalia Neno, ni kumwangalia Yeye. Mwangalie Yeye, Yeye ni Neno, na Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii linafaa kutimizwa siku hii. Wakati wa Nuhu usingalitimizwa siku hii; ulikuwa tu ni mfano, wakati wa Musa, na kadhalika. Lakini hii ndiyo siku ambayo Mungu ameahidi mambo haya ambayo tunafurahia sasa, mambo haya ambayo tunaona sasa, ambayo ulimwengu unayacheka, nguvu hizi kuu za Roho Mtakatifu zinazoweza kubadilisha moyo wa mwenye dhambi, zinazoweza kumchukua mshiriki vuguvugu wa kanisa na kumpa ushuhuda ambao utalitia kanisa moto, kutoka mahali alipotoka. Ni nguvu ndizo ziliingia katika Neno.

80 Kama ambavyo nimesema mara nyingi, nimepata matabaka mawili ya watu. Moja yao ni wa kimsingi; kimahali anajua mahali alipo katika Kristo, kwa sababu ya Neno, bali hana imani yoyote katika yale afanyayo. Hajampokea Roho Mtakatifu. Ndipo ninapata Wapentekoste, wengi wao wamempokea Roho Mtakatifu, bali hawajijui kuwa ni akina nani. Ni kama tu mtu aliye na pesa kwenye benki na hawezi kuandika hundi, na huyo mwingine anaweza kuandika hundi lakini hana pesa kwenye benki. Kama ungaliwaleta hao wawili pamoja, kama ungaliweza kumfanya Mpentekoste atambue kuwa yeye ni nani, na arejee kwenye Neno la Mungu halisi, na kamilifu; pamoja na

huo ubatizo wa Roho Mtakatifu, itautia ulimwengu moto tena pamoja na uamsho mpya wa kipentekoste. Ndugu, dada, hiyo ni kweli.

81 "Niangalieni Mimi, enyi ncha zote za dunia; kwa kuwa mimi ni Mungu, na hapana mwingine kando Yangu."

82 Loo, tunaweza kupambanua ukomunisti, tunaweza kupambanua kila kitu kingine, bali sijui ikiwa tunaweza kupambanua sehemu ya Neno lililotengwa na Mungu kwa ajili ya siku hii? Sijui kama tunaweza kuona ishara ambayo Mungu alituambia ingekuwa hapa duniani katika siku hii? Sijui kama tunaiona?

83 Naam, turudi kwa Musa tena. Alikuwa kabisa. . . alikuwa na mitambo yote kulihusu, lakini siku moja katika kichaka kilichowaka moto, alimsikia Mtu akizungumza kwa sauti ya binadamu, Nguzo ya Moto iliyowaka moto nyuma katika kichaka, akizungumza katika sauti ya binadamu, na kusema, "MIMI NIKO AMBAYE NIKO. Na nimesikia kuugua kwa watu Wangu. Ninalikumbuka Neno Langu, nami nimeshuka kuwakomboa. Nami ninakutuma wewe kufanya hivyo." Ni mtu wa tofauti jinsi gani huyo alikuwa, pindi tu alipopata ninii. . . Alikuwa na mitambo, bali alikuwa na nguvu tendaji ndani yake. "Hakika, nitakuwa pamoja nawe." Hayo ndiyo yote yaliyohitajika kwa ajili ya Musa kwenda, aliangalia na akaona katika kichaka kilichowaka moto.

84 Baadaye katika safari, tunawaona Israeli walipokuwa wakitoka. Waliangalia, pia, nao wakaona nyoka ya shaba. Na katika nyoka hii ya shaba iliyoinuliwa kwa ajili ya magonjwa yao. . . Walikuwa wametenda dhambi, nao wakaona nyoka ya shaba. Katika hii nyoka ya shaba waliona, katika mfano, hukumu ambayo Mungu angeweka juu ya Yesu Kristo, kufa kwa ajili yetu sote wenye dhambi tusiostahili, wenye hatia. Hicho ndicho alichoona.

85 Wanafunzi walimwangalia Yeye, wakati mmoja, wakiwa katika shida, huko nje baharini, nao wakaona nini? Waliona msaada wao. Waliona msaada ukija kupitia Yeye.

86 Martha, siku moja alipokuwa na kifo katika familia, kaka yake mwenyewe alikuwa amefariki, Lazaro, kaka pekee aliyekuwa naye. Alimwangalia wakati wa mauti, naye akaona ufufuo na Uzima. Hicho ndicho alichoona ndani Yake. Sasa, ilionekana kana kwamba Yeye alikuwa amemkataa; alikuwa ameondoka wakati kaka yake alipofariki. Lakini muda si muda wajua, mara moja aligundua. . . Baada ya mvulana huyo kuwa amekufa, na kuzikwa kwa siku nne, alikuwa tayari ananuka.

87 Martha alijua kulikuwako na kitu kumhusu Yeye kilichokuwa tofauti. Alikuwa amesoma Maandiko. Alimwamini Yeye kuwa ni Mwana wa Mungu, Imanueli, Mungu aliyedhihirishwa. Alijua kwamba Yeye alikuwa ni mwakilishi

wa Mungu. Naye alijua, kama Eliya aliweza kumfufua mtoto aliyefariki, na yeye akiwa tu ni sehemu ya Neno, kwa ajili ya wakati huo; Kristo alikuwa ni utimilifu wa Neno, alijua hakika kwamba Yeye alikuwa na nguvu kumfufua kaka yake. Na alipomwendea wakati wa mauti, katika kufiwa, alipata ufufuo na Uzima wakati alipomwangalia Yeye. Hakumwangalia Yeye ili kumkosoa, ama kumwuliza ni kwa nini hakuja, au kumswali.

88 Hupaswi kuliswali Neno la Mungu. Hilo ndilo lililoingiza jamii yote ya wanadamu katika shida, wakati Hawa aliposwali kama Mungu angetimiza Neno Lake lote au la. Nasema usiku wa leo, ndugu zangu, wakati umewadia ambapo lazima tuamini kila Neno aliloandika Mungu. Kila sehemu yake, ni Kweli. "Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

89 Sasa tunaona ya kwamba Mariamu alipata ufufuo na Uzima.

90 Vivyo hivyo Yairo, maskini kuhani, mwaminio wa kisiri, kwamba alipomwona Yesu na kumwangalia Yeye, alipata ufufuo na Uzima.

91 Watu wenye njaa walimwangalia Yeye, siku moja, na wakapata mkate wa kudumisha; mfano kwamba wenye njaa leo hii wanaweza kupata Mkate wa Uzima, si kupata kanuni ya imani. Humpati mwanzilishi, humpati mrekebishaji; unapata Uzima unapompata Kristo, Mkate wa Uzima.

92 Mwizi anayekufa alimwangalia Yeye, katika wakati wa dhiki, naye alipata nini? Alipata msamaha Wake. Ni nani mwingine angalimwangalia? Utawala wa Kirumi usingeweza kumsamehe. Hakuna mwingine yeyote angaliweza kumsamehe. Bali alimwangalia Yesu, katika dhiki yake, ndipo akampata Mtu aliyeweza kumsamehe.

93 Ndugu yangu, dada, usiku wa leo, ikiwa unaning'inia kama alivyokuwa wakati huo, katika mizani ya hukumu; huku ukijua, kama ungekufa, usiku wa leo, kama mshiriki vuguvugu wa kanisa, ama Mpentekoste vuguvugu, ama chochote kile uwezacho kuwa, unajua unakoelekea. Mwangalie Yeye, usiku wa leo, Yule awezaye kukuweka huru. Yule, usiku wa leo, kama wewe ni mshiriki tu, na hujui kile ufufuo wa Kristo unamaanisha kuishi katika moyo wa mwanadamu, mwangalie Yeye. Yeye ni Mungu, na Yeye pekee. Utapata msamaha kama vile huyu maskini, mwizi shupavu, aliyelowa dhambi alivyopata, huku amening'inia Msalabani.

94 Wagonjwa walimwangalia Yeye. Walipata nini? Walimpata Mponyaji. Wagonjwa usiku wa leo bado wanaweza kumwangalia Yeye na kumpata Mponyaji. Walipata katika Yeye kile kilichowakilishwa katika nyoka ya shaba; kama huo ulikuwa ni mfano, hiki kilikuwa ni kitu chenyewe. Vipofu waliangalia na waliweza kuona. "Yeye ni yule jana, leo, na hata milele." Waebrania 13:8.

95 Mshairi aliangalia wakati mmoja, kuona kile angaliweza kuona. Kipofu Fanny Crosby aliangalia wakati mmoja, kuona kile angaliweza kuona. Akiwa kipofu, hili hapa lilikuwa jibu lake:

> Wewe ni Chemchemi ya faraja yangu yote,
> Zaidi ya uhai kwangu,
> Ni nani niliye naye duniani kando Yako?
> Ama ni nani Mbinguni ila Wewe?

96 Eddie Perronet, wakati mmoja, wakati asingaliweza kuuza nyimbo zake naye akashangaa afanye nini. Ndipo akarudi tena ofisini mwake, na huo uvuvio ukamshukia juu yake, Roho Mtakatifu; akanyakua kalamu, akaangalia na akamwona Yeye katika nguvu, kisha akatunga na kuandika wimbo:

> Wote wazisifie Nguvu za Jina la Yesu!
> Malaika na wasujudu;
> Walete taji ya kifalme,
> Na kumvika taji Bwana wa wote.

Hicho ndicho alichoona ndani Yake. Loo, jamani!

97 Petro, mvua samaki wa mahali hapo; wakati ndugu yake alipokuwa akihudhuria uamsho wa Yohana Mbatizaji, Andrea. Walikuwa wakilizungumzia, kuhusu kile Masihi angekuwa, na kulijadili. Baba yake alikuwa amemwambia kwamba, "Kutakuwa na walokole wengi watakaoinuka, kabla tu ya Masihi, bali mtamjua. Yeye atakuwa Nabii. Bwana alisema, 'Yeye atakuwa Nabii.' Tunafahamu kuwaamini manabii wetu."

98 Ndipo hatimaye, siku moja, pamoja na ushawishi wote ambao Andrea angeweza kufanya, hatimaye alimleta Petro kuja kumsikiliza Yeye, kwa sababu alikuwa anaenda kuwa na mkutano huko chini kwenye ukingo wa bahari, asubuhi moja. Aliteremka huko kusikia Neno la Mungu. Na wakati alipotembea kuja Uweponi mwa Yesu Kristo, Petro aliona nini alipomwangalia? Alisema, "Wewe, jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Hilo lilitosha kabisa. Alijua kwamba Neno la Mungu lilikuwa limetimia.

99 Nathanaeli, wakati mmoja, mwaminio halisi katika Agano la Kale, akitazamia kuja kwa Masihi. Aliletwa na Filipo, rafiki yake, katika Uwepo wa Yesu, akisimama jukwaani, kisiki kama sanduku, chochote kile ambacho huenda kikawa, akiwaombea wagonjwa. Ndipo wakati Nathanaeli alipoinga kwenye mstari wa maombi, ama chochote kile kilichokuwa, na kupata kumwangalia Yeye kwa mara ya kwanza, alisikia Sauti ikimrudia, na kusema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake."

100 Akasema, "Rabi, ulinijua lini? Ni lini Wewe ulipata kuniona mimi?"

101 Yeye akasema, "Kabla Filipo hajakuita, wakati nilipokuwa . . . wakati ulipokuwa chini ya mti, nalikuona."

102 Nathanaeli alikiri kuwa aliona nini? Alisema nini? "Wewe ndiwe Kristo. Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli. Wewe ndiwe Mwana wa Mungu." Hilo ndilo aliloona wakati alipoliona Neno la kweli la Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Miaka mia nne bila ya nabii, na kumwona Yeye akitambua mawazo hasa yaliyokuwa moyoni mwake, na yale aliyokuwa amefanya, alijua hicho kisingeweza kuwa chochote pungufu ya Masihi. Hatukuwa tumekuwa nacho, hawakuwa wamekuwa nacho, na kiliahidiwa, na kila mtu alijua wakati ulikuwa umekaribia.

103 Vivyo hivyo tunajua jambo lilo hilo leo hii, tunajua Yesu aliahidi mambo haya. Alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, ndivyo itakavyokuwa wakati atakapokuja." Tunaona mambo haya yakitukia.

104 Unaona nini unapoangalia? Je! unaona, unawazia kuhusu hadithi za kubuni, ama—ama unaona namna fulani ya te—telepathia, ama unawazia nini, kama walivyofanya huko nyuma? Mafarisayo walimwangalia Yeye, walisema nini? "Mtu huyu ana pepo." Watu wale wale wakimwangalia Mtu yule yule, wanadamu: mmoja alimwona Mwana wa Mungu, Neno lililoahidiwa likithibitishwa; na huyo mwingine akaliita ibilisi. Unaona nini? Unaangalia nini leo wakati unapoona nguvu za Roho Mtakatifu zikienea katika jengo, zikitimiza ahadi Yake kwamba katika siku hizi za mwisho kile Yeye angefanya? Unaona nini unapoangalia? Kama ukiona Neno la Mungu likithibitishwa, basi ni Roho Mtakatifu wa Mungu. Naam, bwana.

105 Nathanaeli aliliona Neno lililoahidiwa alilokuwa ameliishia, kuiona ahadi iliyopakwa mafuta ikifanyika mwili. Musa, nabii, alikuwa amesema hivyo. Huyo Musa, nabii aliyetiwa mafuta, alikuwa ameliahidi Neno hilo.

Mwanamke kisimani, siku moja.

106 Watu wengi walikuwa wamemkataa. Mafarisayo na Masadukayo walikuwa wamemwita "pepo." Walisema, "Alifanya hili kwa upiga ramli. Alikuwa ni roho mwovu. Alikuwa ni mwendawazimu. Alikuwa hana mahali pa kwenda; hiyo ndiyo iliyokuwa shida Yake, kwamba Yeye alikuwa tu ni mtu ha—haini."

107 Nini kilitokea? Nini kilitokea? Alipitia Samaria, na mji wa Sikari. Ndipo wakati alipoenda huko nje, siku moja, na kuketi chini juu ya ma—maskini mandhari pale. Kulikuwako na mwanamke aliyekuja kupata maji ya kunywa, naye akasema . . . Na Yeye akamsikia. Mwanamke alisikia Sauti ikisema, "Nipe maji ninywe, ewe mwanamke." Ndipo Yeye . . . Mwanamke akaangalia, aliona nini?

108 Kwanza, asingeweza kulielewa. Akamwuliza. “Si desturi kwenu ninyi Wasamaria ku—kuomba, ama ninyi Wayahudi kuwaomba Wasamaria hivyo.”

Kasema, “Lakini, mwanamke, laiti ungalijua ni Nani ulikuwa ukizungumza naye!”

109 Sasa kumbukeni, kulikuwako na Nuru ndogo, mbegu ya Uzima imelala pale, ilikuwa imechaguliwa tangu msingi wa ulimwengu. Alikuwa akitazamia Hiyo. Alikuwa amechoshwa na theolojia yao yote na upuuzi waliokuwa wamesema. Lakini alikuwa anatazamia kitu fulani, maana alijua kwamba kulikuwa kunakuja Masihi.

Ndipo Yeye akasema, “Nenda kamwite mume wako mje hapa.”

Mwanamke akasema, “Sina yeyote.”

Kasema, “Umesema kweli. Umekuwa na watano.”

110 Upesi, maskini mbegu hiyo ikachipuka kwa Uzima. Aliona nini? Aliona ishara ya Masihi, katika Mtu. Aliona Neno lililoahidiwa likidhihirishwa. Akasema, “Bwana, naona kuwa Wewe ni nabii. Hatujakuwa na mmoja kwa mamia ya miaka. Tunajua kwamba tumeahidiwa kuwa Masihi yuaja, na, wakati akija, Yeye atatuambia haya. Hilo ndilo atakalofanya.” Mnaona? Aliona nini, aliona nini? Aliona ishara iliyoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo, ikidhihirishwa.

111 Roho Mtakatifu ameahidiwa kwa ajili ya siku hii, nguvu za kufufuka Kwake, Kanisa, kwamba, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Yesu aliahidi, “Na mambo nifanyayo nanyi pia mtayafanya.” Unaangalia nini unapoona?

112 Unapoenda kanisani Jumapili asubuhi, je! unaangalia kuona kinanda kizuri, mhudumu aliyevalia nadhifu, kwaya iliyovaa majoho, kundi la wanawake waliojipaka rangi? Unaangalia nini, namna fulani ya chama makanisani? Wewe ni mshiriki wa *hiki* na *kile*. Unaangalia nini? Ni kama hicho ndicho unachoona. Sikilizeni hapa. Si ajabu, unapobeba Injili chapwa, na kumwona Roho Mtakatifu akija na kuidhihirisha miongoni mwa kundi la watu wa mtindo wa kale, ni geni kwako, ni vigumu kwako kuamini.

113 Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, kumhusu Yusufu, “Ilikuwa ni vigumu kwake kuwazia kumhusu Mariamu kuwa na mimba. ‘Angewezaje kuwa hivyo, maskini mwanamke mtakatifu namna hiyo, naye alisema Gabrieli alikuwa amemtembelea?’” Lakini lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida sana. Ilikuwa si kawaida sana kwa jambo kama hilo. Halikuwahi kutukia hapo kabla.

114 Hapo ndipo Mungu anaishi, katika mambo yasiyo kawaida, kwa akili ya kimwili. Lakini wale wanaomwamini Yeye kuwa ni yule yule jana, leo, na hata milele, mambo yote yanawezekana.

Kila Neno aliloahidi litatimia. Ni mambo yasiyo ya kawaida ndiyo humfanya Yeye kuwa Mungu. Yeye huenda kwa yasiyo kawaida. Yeye hufanya kila kitu kisicho kawaida kwa watu. Naam, bwana. Vema.

115 Mwanamke huyo alimwangalia, naye akaiona ishara ya Masihi, Mungu akidhihirishwa katika mwili. Wengi, watu wale wale, waliangalia nao hawakuona chochote.

116 Wasioamini katika siku za Nuhu, waliona nini? Mlokole, akitengeneza kwa kubabaika katika kile alichokiita kuwa mashua. Hayo ndiyo yote waliyoona. Huku, mashua hiyo yenyewe ilitengenezwa kwa ono kutoka kwa Mungu Mwenyezi. Kitu kile kile alichokuwa akijenga, ujumbe wake aliokuwa akihubiri, alikuwa akijenga kwa ujumbe wake, akishuhudia kwamba alikuwa mwenye haki na alikuwa akitazamia mbele. Aliishi kile alichohubiri.

117 Hilo ndilo tunalopaswa kufanya leo hii. Hakuna mtu aliye na haki kuhubiri mpaka amejazwa na Roho Mtakatifu. Kweli! Wanatheolojia na wanahisabati, na kadhalika, wanaweza kulieleza Hilo na kuliweka mbali na wewe. Lakini iwapo mtu amewahi kuwa upande wa nyuma ya jangwa, mahali pale patakatifu, na kukutana na Mungu kama Musa alivyofanya, hakuna mtu awezaye kuliondoa hilo kwake. Anajua! Yeye ndiye aliyekuwa huko. Hakuna mtu awezaye kumwambia lolote juu yake. Alikuwa huko. Hiyo ndiyo sababu Yesu aliwaagiza wanafunzi Wake, "Msihubiri mpaka mwende kwenye mji wa Yerusalemu na kupokea Nguvu kutoka Juu, ndipo mtakapokuwa mashahidi Wangu." Hilo ndilo waliloona. Naam, bwana.

118 Nuhu. Wasingeweza kuona chochote; walifanya nini baada ya kufanya hilo? Walipuuza Neno la Mungu na kuleta hukumu juu yao wenyewe. Hiyo ni kweli.

119 Ninasema, pamoja na Jack Moore, sio kumnukuu, bali nasema hili, kwa kuwa nafikiri ni majira yafaayo sasa. Jack Moore alisema, "Mungu asipoizamisha Marekani na kuiteketeza, itambidi kuinua Sodoma na Gomora na kuomba msamaha kwa kuwachoma moto." Na hiyo ni kweli.

120 Mungu ni mwenye haki. Neno Lake lina ujira wa haki, na Yeye hakika atauhukumu ulimwengu kwa matendo yake dhidi ya Neno Lake leo hii. Haijalishi ni mikutano mingapi tuliyo nayo, ni mikutano mingapi ya kidini tuliyo nayo, hilo silo. Neno hili!

121 Angalieni, hakuna nyakati za kidini zaidi ya ilivyokuwa siku ile ambapo Yesu alikuja duniani, loo, kila kitu kilimezwa katika dini na mapokeo, na yote ni makosa!

122 Ndivyo ilivyokuwa wakati Amosi, maskini mhubiri mwenye kipara; hatujui alikotokea. Macho yake mawili madogo yalisinyaa wakati alipopanda akavuka kilima na kuangalia ndani ya Samaria. Ulikuwa ni mji mkuu wa watalii, kama vile Phoenix. Wengi wa watu walikuja kutoka kote ulimwenguni,

kuangalia, kuuona mji huu mkuu, jinsi ulivyokuwa wa kupendeza. Loo, kila kitu kilikuwa kinandelea, vilabu vya usiku na mahali hasa pa anasa, "mahali pa kuishi," walisema. Lakini wakati maskini mvulana huyu mkulima, aliposhikwa na Roho Mtakatifu, akashuka kupitia pale, hakuwa na mtu wa kutangulia na kufanya maandalizi kwa ajili ya mikutano yake, hakuwa na ubao wowote wa kutangazia, hakuna dhehebu la kushirikiana naye, wala mtu yeyote wa kumwunga mkono. Lakini alipotembea kukivuka kilima na kufinya macho hayo madogo, wakati alipouangalia mji huo, aliona kitu ambacho hakuna mmoja wa hao wengine aliyeona. Wote waliona anasa na kadhalika ya mji huo. Lakini yeye aliona hukumu ya Mungu inayongojea, na akatabiri dhidi yake. Wakamwita "mwendawazimu." Lakini miaka kumi na moja baadaye, ilitendeka hasa jinsi alivyosema.

123 Mtu anayeweza kuangalia kanisa jinsi linavyoenenda leo hii, na watu jinsi wanavyoenenda, na kubashiri baraka siku za usoni? Nabashiri hukumu, hiyo pekee. Mungu mwenye haki anahitaji hukumu, kwa kulipuuza Neno Lake. Yeye ana haki kuja na kutambulisha Hilo mbele zetu, na kulifanya sahihi. Lakini Mungu mwenye haki, kupitia nyakati zote, Yeye hawezi kubadilisha mpango Wake. Kamwe habadilishi mpango Wake. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Njia Zake ni zile zile. Neno Lake ni lile lile. Kote, Yeye ni yule yule. Amejawa rehema wakati mtu yuko tayari kutubu, bali hukumu itafuata usipotubu.

124 Farao, wakati alipoangalia, na aliyedhaniwa kuwa mlokole, aliyedhaniwa kuwa ni nabii mlokole, akiwa na madai mengi ya ukombozi, hayo ndiyo yote aliyoona. Lakini Waisraeli waliona mkono wa Mungu juu ya Musa. Naam, bwana.

125 Yule mtu tajiri aliangalia na kuona, alikuwa na uwezo, lakini dhehebu lake lilikuwa kuu zaidi ya kile angeweza kupitia pamoja na Hilo. Mtazamo wake unaofuata ni wapi? Aliangalia kutoka kuzimu. Hiyo ni kweli kabisa. Hukumu ilimjia. Huo ndio wakati mwingine alipoangalia. Ndivyo itakavyokuwa na watu wengi leo hii.

126 Askari wa Kirumi aliangalia, wakati mmoja, walipomsulubisha Yesu. Aliangalia aweze kuona kile Yeye alikuwa amefanya, bali ilikuwa imechelewa sana wakati huo.

127 Marafiki, Marekani itafanya hivyo, pia. Wataangalia siku moja, na kusema, "Kwa kweli huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu," ila itakuwa imechelewa sana. Walikuwa wamecheka na kudhihaki kwa mara ya mwisho.

128 Angaliweza tu kuangalia wakati huo na kuona mahali ambapo angaliweza kuokolewa, lakini ilikuwa imechelewa sana wakati huo. Alikuwa amemsulubisha Mkuu wa Uzima.

129 Na mara nyingi sana, leo hii, watu humkataa Yesu Kristo mioyoni mwao, wakati wamemwona Yeye akithibitisha wazi

kuwa Yeye ni Nani, moja kwa moja miongoni mwetu. Naam, bwana.

130 Pilato aliangalia, siku moja, na alishawishika, lakini siasa zake zilikuwa kuu sana. Asingeweza kabisa, asingelitetea.

131 Luther aliangalia, naye akaona kuhesabiwa haki. Akaenda na hilo. Ndipo wakaunda dhehebu.

132 Wesley akaja, akaona utakaso alipomwangalia Kristo, kwamba kanisa linapaswa kutakaswa. Na akaenda moja kwa moja na utaka-. . .

133 Pentekoste ikaja na kuona kurejeshwa kwa vipawa. Wote walifanya nini? Kama tu Wakatoliki walivyofanya, wakaliundia dhehebu, wakaliweka moja kwa moja huko nyuma.

134 Ee Mungu! Siku moja niliangalia, na, nilipoangalia, niliona Alfa na Omega. Niliona Mwanzo na Mwisho. Nilimwona Yesu Kristo yeye yule jana na . . . Niliona Mwenye kusamehe dhambi zangu. Nilimwona Mtu aliyechukua mahali pangu. Jamani!

Mnaona nini mnapoangalia?

135 Ninamwangalia sasa hivi rafiki yangu wa kale, Bill Dauch, anayeketi hapa. Mtu huyo sasa anafikisha umri wa miaka tisini na mbili. Siku chache zilizopita, si muda mrefu uliopita, hasa, yapata miezi sita iliyopita, alikuwa na kusita kabisa kwa moyo na mshtuko wa moyo, pamoja.

136 "Daktari anasema yuafa." Mke wake akaniita na kusema, "Ndugu Branham, njoo. Anakufa. Bill ni rafiki yako."

Nami nikasema, "Vema, nitafanya hivyo."

137 Basi nikiwa njiani nikielekea kwake, nilikuwa nikiomba. "Mungu, ninachukia kuenda kumwambia 'kwaheri.' Ninajua kama angaliishi tu mpaka nifike huko, kwamba ninaweza kumwambia 'kwaheri.'" Chini ya oksijeni, moyo kusita kabisa, umri wa miaka tisini na moja. Nilitoka nje kwenye kituo cha petroli, ndipo nikaangalia, na, nilipoangalia, nilimwona Bill akiteremka barabarani na kunipa mkono.

138 Huyu hapa ameketi usiku wa leo. Daktari aliyemwambia hilo, amekufa. Na hapa ameketi Bill Dauch mwenyewe, kutoka Lima, Ohio, akiendesha motokaa kupitia kwenye mvua ya theluji na theluji, akifuata kila mkutano niendao. Kwa nini? Tuliangalia; tukaona kitu fulani. Mungu yeye yule niliyenena juu yake jana usiku, huko Colorado, wakati wa dhoruba, niliangalia, nikaona ya kwamba Yeye alikuwa ni yule yule jana, leo, na hata milele.

139 Hapa ameketi Bw. Way, Mwingereza, ameketi hapa pembeni, papa hapa sasa, ndiyo kwanza nimwone ameketi hapa. Amekuja kutoka Indiana. Yeye ni Mwingereza. Mke wake ni m—mwuguzi aliyesajiliwa. Mtu mzuri! Siku moja, nilizungumza naye. Nilikuwa nikihubiri kwenye mkutano, akachukizwa na

yale niliyosema, moyoni mwake, na, alipochukizwa, alianguka akafa moja kwa moja kwenye kusanyiko. Hapo akafa. Mke wake akamshika na kumhisi; macho yake, uso ukawa mweusi, macho yake . . . si kujifanya, macho yake yakajitokeza na kuenda nyuma huko nyuma ya kichwa chake. Nikasema, "Simama kwa utulivu." Nikamwangalia pale chini, na kuwazia, "Loo, huyo hapo mtu huyo amelala, amekufa."

140 Nikashuka chini, nikaweka mikono yangu juu yake, alikuwa baridi tu kama hilo dawati lilivyo. Alikuwa ameenda. Bibi Way akasema, "Loo, Ndugu Branham, ameenda! Ameenda." Akipiga mayowe kwa sauti kuu alivyoweza.

141 Nikaangalia kando. Nikaona ufufuo na Uzima. Nikaomba maombi ambayo Yesu aliniambia niombe, ndipo Ndugu Way akafufuka. Hapa ameketi papa hapa usiku wa leo, amefufuka kutoka kwa wafu, ameketi papa hapa usiku wa leo.

142 Hiyo ni kweli, Bw. Way, kama utasimama tu kwa dakika moja, kusudi watu waone. Naye huyu hapa Bill Dauch ameketi *hapa*.

143 Ni kitu gani? Kwa sababu tunamwangalia Yeye ambaye ni yule yule aliyemfufua Lazaro, Yeye ni yule yule kama alivyokuwa. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Naam, Yeye habadiliki.

144 Huyu hapa ameketi maskini mhubiri mbele yangu, jina lake Blair. Mvulana wake mdogo alikuwa kwenye ajali hivi majuzi, na mke wake ameketi pale, wakiyapangusa machozi macho yao sasa. Waliniita kwa simu huko chini, naye akasema, "Ndugu Branham, mvulana wetu mdogo alikuwa kwenye motokaa na akagonga kilima, naye amepondwa, akajeruhiwa ubongo wake, na kila kitu. Amekwisha, karibu hivyo; anapumua kwa shida." Kasema, "Utaomba?"

Nikasema, "Hebu tuombe."

145 Nikaanza, nikaangalia, hii kwenye simu, nikaanza kuomba. Nikasema, "Bwana Mungu, nitawaambia nini?" Nikamwona mvulana mdogo akienda, akikimbia na kuruka kamba, akikimbia huko namna hiyo. Nikasema, "Atakuwa mzima." Naye huyu hapa usiku wa leo. Na hapa wameketi hapa. Kwa nini? Kwa sababu Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

146 Angalia! Angalia! Unaona nini unapomwona Yeye? Ninamwona Mponyaji yule yule. Amina. Ninamwona Mtu yule yule aliyetembea Galilaya. Ninamwona katika nguvu Zake. Ninamwona akitambua mawazo na siri za moyoni, akionyesha—akionyesha ishara kabla tu ya wakati wa mwisho. Jinsi ambavyo tungeweza kupitia kusanyiko hili na kote katika mataifa, tukisema kile alicho Yeye leo hii!

147 Unajua kile ninachowazia? Kama vile maskini Mmarekani mweusi alivyosema wakati mmoja, wakati wa utumwa. Siku moja, alikuja, akasema, "Unajua, ninii . . . niko huru sasa." Kwa hiyo akaanza kusema miongoni mwa watumwa wengine, nao watumwa wakasema . . .

148 Na likamrudia tajiri wao. Naye tajiri wao akasema, "Njoo hapa ndani, Sam." Kasema, "Ni nini hicho unachosema miongoni mwa watumwa huko nje?"

Akasema, "Bosi, niko huru."

Kasema, "Uko huru kwa njia gani?"

149 Akasema, "Niko huru kutokana na sheria ya dhambi na mauti, kwani Yesu Kristo ameniweka huru."

Akasema, "Sam, unamaanisha hilo?"

Akasema, "Naam."

150 Kasema, "Nitashuka niende nikatie sahihi kuachiliwa kwako, na kukuacha uende ukawaambie ndugu zako kuhusu hilo."

151 Mzee huyo akahubiri miaka na miaka. Hatimaye, siku moja, akafikia mlango wake, ilimbidi kuyaondokea maisha haya. Basi wakati alipokuwa amelala kwenye kitanda chake, katika hali ya kuzimia roho kwa siku chache, wengi wa ndugu zake wazungu wakaja ku—kumwona, kumwaga kwaheri, kwa sababu alikuwa ni maskini askari hodari wa Kristo. Wakati akiwa amelala pale kitandani, akafikia, akaangalia kote, ndipo akasema, "Mose, hivi wewe si, au . . . "

"Sam, hujaondoka bado?"

152 "La." Kasema, "Ilinibidi kurudi." Akasema "Nilidhania nilikuwa kule." Kasema, "Ha—ha—hapana shaka niliota hilo." Kasema, "Nilidhani nilikuwa kule. Na wakati nilipokuwa nimesimama huko," kasema, "Malaika fulani . . . nilikuwa tu nimeingizwa mlangoni, ndipo," kasema, "Malaika fulani akaja na kusema, 'Sam, njoo ukapokee taji yako, na uje upokee joho lako.'"

153 Akasema, "Usiniambie kuhusu taji na joho, hebu niruhusu tu nisimame hapa na kumtazama Yeye kwa miaka milioni moja." Aliona katika Yeye Mtu yule aliyekuwa amemweka huru kutokana na dhambi na mauti. Aliona pale Yule aliyempigania kwa heri na kwa shari. Ee Mungu!

154 Hivi majuzi asubuhi, nilikuwa nimelala kitandani mwangu. Nilizoea kuwa na . . . Mnajua hadithi ya maisha yangu. Nilikuwa na maskini mbwa, tulimwita Fritz. Alinipeleka shuleni; mahali kindi wamejificha, na kadhalika. Vema, nilizoea kumchukua kila asubuhi. Ningepanda, orofa ya juu, kwenye maskini nyumba ya magogo, ningemsikia akibweka huko chini kwenye shimo.

Kamwe hakunidanganya. Siku zote nilipomwendea; alikuwa na kitu kwa ajili yangu.

155 Mnajua, mojawepo ya asubuhi hizi, nitamsikia akibweka huko kwenye pango. Lazima niende nione kuwa ana nini. Itakuwa sawa.

156 Sikiliza, ndugu, hebu nikwambie. Kuna kitu kimoja tu cha kuangalia unapomwona Yesu Kristo, hiyo ni kumwona Mungu ndani Yake, yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninaamini Yeye yupo hapa, usiku wa leo, kutufanyia kama vile alivyofanya wakati ule.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi, tunapoomba. Omba!

157 Je! kuna mmoja humu ndani, usiku wa leo, angesema, "Ndugu Branham, mwombe Mungu anirehemu. Ninataka kuangalia na kumwona tofauti. Nimemwangalia na kubahatisha. Nimemwangalia na kushangaa. Nimemwangalia na kuswali. Je! kwa kweli, alinijali? Je! ananipenda? Mambo haya yote yaliyosemwa juu Yake, je! ni ya kweli? Ninataka kujua kama ni kweli. Je! utamwomba anifunulie usiku wa leo?" Waweza kuinua mkono wako? Bwana akubariki. Hilo ni jema. Kila mahali.

158 Bwana wa thamani kuna mengi sana yaliyoandikwa kukuhusu. Tunajua kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tunaomba, Bwana, kwamba, usiku wa leo, tunapoangalia, kwamba tutamwona Yesu Kristo. Uliahidi katika Neno Lako, kwamba, kazi ulizofanya Wewe, sisi nasi tungezifanya. Uliahidi, katika siku za mwisho, kwamba Wewe ungerudi hapa duniani, katika umbo la Roho Mtakatifu, kanisa lingejaa nguvu, Roho Mtakatifu. Ulisema, "Bado kitambo kidogo, na haitafaidia ulimwengu kitu kuangalia, maana hawatamwona. Bali ninyi mtamwona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi ukamilifu."

159 Bwana Yesu, wakati kungali na nafasi kwa mwanadamu kuangalia, jalia waangalie usiku wa leo na kumwona Yeye katika nguvu za kufufuka Kwake. Yeye hajafa, bali yu hai milele, tayari kuwaombea wale walio tayari kumkiri Yeye. Tujalie, Bwana. Na jalia haja hizi zote, ambazo zimeombwa, zitimizwe. Baba, yajalie mambo haya, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

160 Sasa ni wakati wa maombi kwa ajili ya wagonjwa. Niliwaombeeni, aminini kwamba Mungu atajibu.

161 Sasa, ninaamini Billy alisema alisambaza kadi zaidi za maombi. Zilikuwa ni za B? Za B. Vema. Hatuna wakati; nilipitiliza wakati kidogo; samahani. Ninazo dakika chache tu. B, ni wapi tulipo—ni wapi tulipoachia, kwenye hizo, jana usiku? Tuliachia wapi, tuliachia wapi jana usiku? [Mtu fulani anasema, "Tulizichukua zote."—Mh.] Loo, tilichukua zote? Tutaanzia tu kwenye B, namba moja, basi. Vema.

162 Namba moja, nani . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . tatu, nne, tano.

163 Mtu fulani aangalie sasa. Shuka hapa chini, Billy, baadhi yenu, upesi sana, maana hatuna wakati sasa. Tuninii tu . . . wala tusichukue wakati. Wakati mwingine ni viziwi na hawawezi kusikia, na, ama labda hawawezi kusimama, ama kitu kama hicho. Ikiwa wako hivyo, mbona, sisi . . .

164 Namba moja, mbili, tatu, nne, tano. Vema, njoo hapa mbele, kama unaweza. Kuna mmoja, wawili, watatu, wanne . . . Hiyo ni kweli. Samahani, bwana. Sita, saba, nane, tisa, kumi, hebu wasimame sasa. Sita, saba, nane, mtu fulani sasa, nane, tisa, kumi. Nane, tisa . . . Vema. Moja, mbili, tatu, nne, tano . . . saba, nane, tisa, kumi. Vema, kumi hadi kumi na tano, simameni; katika B, vema, hizo ndizo kadi zote zilizosambazwa. Kumi na tano, vema, kumi na tano hadi ishirini, simameni. Moja hadi ishirini, katika kadi za maombi, chukueni mahali penu *hapa*. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa. Ndilo hilo. Ishirini hadi ishirini na tano.

165 Ni wangapi wasio na kadi ya maombi? Ungali unamwamini. Wakati wanapokuja, wakichukua mahali pao, wakati hao ishirini na watano wanapokuja, ishirini na tano wa kwanza wanapokuja, hebu niwaulize. Biblia ilisema, katika Kitabu cha Waebrania, kwamba "Yesu Kristo ni Kuhani wetu Mkuu." Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Anayewezwa kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Je! tunaenda kuketi, katika siku hii, bila ya furaha; na kumwona Kuhani wetu Mkuu mashuhuri akijitambulisha Mwenyewe miongoni mwetu, halafu tuketi kama ng'ombe bubu wanaofukuzwa? La, bwana. Hebu na tuwe wachangamfu na tukitenda, tukiwa na moyo kwa ajili ya ugomvi wowote. Usiwe kama ng'ombe bubu wanaofukuzwa. Kuwa shujaa! Enyi watu angalieni huku na mwamini. Angalia kwenye Maandiko, kile ambacho Yeye aliahidi. Vema.

Hatutachukua wakati wowote, tutaanza moja kwa moja kwenye mstari wa maombi.

Hebu na tuombe tena.

166 Bwana Yesu, yako mkononi Mwako sasa. Niko mkononi Mwako. Bwana, litwae Neno ambalo Wewe ulisema, "kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," lile nililorejea usiku wa leo. Ulisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, wakati ulipokuwa ukiwazungumzia wanafunzi Wako kuhusu kuondoka, Wewe ulisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya."

167 Biblia ilisema kwamba, "Mungu, zamani za kale na kwa njia mbali mbali alinena na manabii, ama, alinena na baba zetu

kupitia manabii; katika siku hizi za mwisho kupitia Mwanawe, Yesu Kristo." Na Yeye ni Neno. Tunajua kwamba manabii walikuja, Roho alikuja juu yao na kulifanya hilo Neno liishi kwa ajili ya kizazi hicho; wakawalaani wafalme, wakaleta hukumu, wakaleta haki, wakaokoa waliopotea; manabii waliojiliwa na Neno.

168 Sasa katika siku hii ya mwisho, Bwana, Wewe uliahidi. Ulisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," wakati Ibrahimu alikuwa ameketi pale kwenye joto la mchana, maskini, Kanisa dogo lililoitwa litoke. Tunaangalia kote uimwenguni leo, Baba, tunaona Sodoma hasa, Wamataifa waliopotoshwa, vuguvugu. Pia tunaona hawa malaika watatu wakitokea mbele ya Ibrahimu.

169 Wawili kati yao waliteremka kwenda kwenye kanisa vuguvugu, Lutu, kujaribu kuwaita watoke. Wawili waliteremka kule, Billy Graham wa kisasa, kuwaita watoke; hakuna miujiza, alipofusha tu macho yao. Kuhubiri Injili hufanya hivyo.

170 Lakini kulikuwako Mmoja aliyekaa huko juu kwenye kundi la Ibrahimu, akionyesha wateule, walioitwa watoke, ambao hawakuwa Sodoma; walizaliwa, nje ya Sodoma, Kanisa la kweli, Uzao wa Ibrahimu wa siku ya leo. Basi wakati Mtu huyu, aliyewazungumzia, kasema, "Yu wapi Sara, mkeo?"

Kasema, "Yuko hemani nyuma Yako."

171 Ndipo akasema, "Nitakuzuru kulingana na majira ya maisha." Naye akacheka.

172 Akasema, "Ni kwa nini akacheka?" Akatambua kile alichokuwa akisema na kuwazia ndani yake, huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema ambapo yeye alikuwa.

173 Yesu wa Nazareti, Mwana wa Mungu, ametuambia katika Neno Lake, "Kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

174 Na ni jambo la kigeni sana, Baba, kwamba hakujawahi kuwa na mrekebishaji, katika nyakati zote, ambaye amewahi kwenda Sodoma, mwenye jina linaloishia "h-a-m," mpaka leo. Mtumishi Wako, Billy Graham, huko chini Sodoma akifanya kazi yake.

175 Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utaokoa Uzao wa Ibrahimu uliopo hapa usiku wa leo, wajaze na Roho Mtakatifu wa Mwana wa thamani aliyeahidiwa. Punde baada ya hapa, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili alifanya ishara hii, ndipo mwana aliyeahidiwa akajitokeza jukwaani. Mungu, tumekuwa tukimtazamia Huyo kwa miaka elfu mbili, Uzao wa Ibrahimu. Wengi wanalala; hii ni zamu ya saba, tunakitazamia kile kilio kuja wakati wowote, "Tazameni, Bwana-arusi yuaja."

176 Tujalie, usiku wa leo, Baba, kwamba ufahamu wa watu utafunguliwa, kwamba wataona kuwa ishara hii iliahidiwa, kabla tu ya kuja kwa Mwana. Vile vile, kama nyoka wa shaba

ilivyomwakilisha Kristo, ndivyo na kuja kwa mwana na ishara ya kuja kwake (katika hali ya kawaida) kunafananisha ule wa kiroho, kwa kuja kwa Yesu leo hii, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Tujalie, Bwana. Tunaomba katika Jina la Yesu, huku tukijikabidhi Kwako. Amina.

177 Ningependa kusema jambo moja kabla tu hatujawaombea wagonjwa. Watu wengi wana dhana potovu kuhusu karama. Karama si kitu ambacho Mungu hukupa kuenda nje na kusema, "Hapa, nitaenda hapa na nichukue *hili*, na nitachukua lile na nitafanya *hili*." Hizo si karama. Watu wengi sana hufikiria hilo, lakini wamewazia visivyo. Karama ya Mungu ni kujua tu jinsi ya kujiondoa mwenyewe njiani kusudi Mungu aweze kukutumia, hayo tu ndiyo karama. Mnaona? Mradi tu uko katika nafsi yako . . .

178 Hivi si Yesu alisema, Mwenyewe, "Mwana anaweza kufanya . . . " Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe." Alipitia karibu na lile birika ambapo walemavu wote walikuwa, na kumponya mtu mmoja mwenye tatizo la tezi dume, ama kitu kingine (ugonjwa) aliyedumaa. Akasema "Mwana hawezi kutenda neno lolote Mwenyewe; ila lile amwonalo Baba akitenda, hilo atenda Mwana vile vile." "Si mimi," Yeye akasema, "nifanyaye kazi hizi; ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu, Yeye ndiye huzifanya Kazi."

179 Sasa, enyi watu mlioketi hapo nje, msithubuti kumwangalia mtu yeyote. Mwangalieni Kristo; Yeye Ndiye. Lakini aliahidi katika siku za mwisho kwamba Yeye atajidhihirisha Mwenyewe katika mwili wa binadamu, kama alivyofanya huko Sodoma. Sasa mwili wako, mwili wangu, hebu na tufungue tu mioyo yetu na tuondolee mbali wazo letu wenyewe, na tuliache Neno lichukue njia Yake, usiku wa leo, ndani yetu, ndipo tutaona karama kuu za Mungu za Roho Wake zikidhihirishwa mbele zetu.

180 Iweni na kicho kabisa. Mtu yeyote asiondoke. Tulieni kabisa na mwombe. Nina hakika mnathamini.

181 Na endapo kuna mtu yeyote hapa anayefikiria huu ni udanganyifu, nakupa changamoto uje mimbarani. Yeyote! Halafu, kama unaogopa kufanya hivyo, usiseme chochote juu yake.

182 Katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho hapa ndani, chini ya udhibiti wangu, kulitangaza Neno la Mungu.

183 Hii hapa picha usiku wa leo, kama vile Yohana Mtakatifu mlango wa 4. Mwanamume na mwanamke wanakutana pamoja, nadhani kwa mara ya kwanza. Sikujui. Labda unanijua, kwa magazeti na—na uvumi, bali mimi sikujui. Unajua hilo. Hatufahamiani moja na mwenzake, kama vile Bwana wetu alivyokutana na mwanamke wakati mmoja kisimani; mwanamume na mwanamke wakikutana, wakizungumza.

184 Lakini kama nikija kama mmoja wa baadhi ya ndugu zetu, ningesema, "Mungu alinipa karama ya uponyaji, . . . "

185 Unajua karama ya uponyaji ni nini? Imani katika uponyaji. Unaona, wewe achilia tu imani yako, kumwombea mtu, hiyo ndiyo yote iliyo karama ya uponyaji. Kila mhudumu anapaswa kuwa nayo, kila mtu, mnaona, anapaswa kuwa na karama ya uponyaji. Nguvu zinazokuponya ziko ndani yako, Roho Mtakatifu, huna budi tu kumwacha awe na njia Yake ya kutokea. Ni hayo tu.

186 Kama tu vile uhai ulioko ndani ya mti. Haikubidi kumimina matofaa ndani ya mti, kuufanya uzae matofaa. Unapandwa tu ardhini, nao unakunywa na kusukuma.

187 Vema, hivyo ndivyo unavyofanya Roho Mtakatifu. Yuko ndani yako. Unakunywa tu kutoka kwenye chemchemi isiyomalizika ya Yesu Kristo, Naye anasukuma nje matunda ya Roho. Mnaona?

188 Sasa nimesimama hapa, bila kukujua. Mungu anajua hilo. Wewe ni mgeni kabisa.

189 Sasa kama ningalienda nikuwekee mikono, na kusema, "Dada, utapona." Ungeweza kuamini hilo, na hiyo ingekuwa sawa. Lakini sasa vipi kama Yeye akija . . . Unaona, hiyo ilikuwa siku zilizopita, huko nyuma katika siku za Pentekoste.

190 Tunaishi mbali na hiyo sasa. Tumeenda zaidi ya Pentekoste, kama vile sisi ni Wamethodisti na Walutheri. Tuko huku mbali kwenye kuja kwa Bwana, ambapo huduma ambayo Yesu Kristo aliifanyia kazi, Mwenyewe, haina budi kuwa sawa hasa. Kama vile jiwe la kichwa juu ya piramidi, halina budi kuchongoka sana mpaka kila jiwe litoshee kikamilifu. Nalo kanisa halina budi kuingia katika hali hiyo ili kupokea Jiwe la Kichwa, kisha lichukue kila kitu katika ufufuo, Mwili utakapofufuliwa.

191 Je! mnaamini hilo? Mnaamini mambo haya ninayowaambieni kwamba ni kweli? Mnaamini? Iwapo Bwana Yesu ataniambia jambo fulani ambalo umefanya, jambo ambalo hukupaswa kufanya, jambo lililo shida yako, ama chochote kile, la kifedha, kinyumbani, sijui; chochote kile, utaniamini, je! utaniamini, kuwa ni mtumishi Wake?

192 Wewe ni Mkristo. Unaona, nilinena nawe ili tu kupata roho yako. Unaona, hivyo ndivyo Yeye alivyofanya jambo hilo pale kisimani; akasema, "Niletee maji ninywe." Wewe ni Mkristo. Wewe ni mwaminio. Hiyo ni kweli. Si mwomba lifti; mwaminio! Vema. Shida yako, shida yako kuu, iko shingoni mwako. Nyuma ya shingo yako, una kivimbe, na kivimbe hicho kinakutia presha. Kinaharibu macho yako, na kadhalika. Je! hiyo ni kweli? Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Kama utaamini, kitaondoka. [Dada huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Mungu akubariki. Enda sasa.

193 U hali gani, bwana? Sikujui. Hatufahamiani mmoja na mwenzake. Yesu Kristo ni yeye yule ja-. . .leo, na hata milele. Kama ninaweza kujiachilia, vya kutosha hivi Roho Mtakatifu anaweza kutumia midomo yangu na macho yangu, kama tu vile. . .

194 Je! uliwahi kuota ndoto? Hakika. Kuna se—sehemu yako, inakubidi uwe umelala katika hisia zako tano. Una—una dhamira ya kwanza na dhamira ya ndani. Dhamira yako ya kwanza ipo *hapa*, na dhamira yako ya ndani ipo mahali *hapa*. Inakubidi uwe umelala katika hisia zako tano, kuenda *hapa* ili kuota ndoto; lakini unaporudi, inavuta hii mpaka unakumbuka kile ulichoota.

195 Sasa, waonaji, manabii, dhamira yao ya ndani haiko *kule*; ipo papa *hapa*. Hutoki katika hisia zako tano; unasimama, umesimama, ukiota. Na ungesema ota. . .Ningesema, "Niotee ndoto." Usingeweza kufanya hivyo. Wala nami siwezi kukuonea ono. Inahitaji Mungu kufanya hivyo. Lakini, siendi kulala ili kuona ono, ninasimama hapa na kuliona. Hiyo ni karama ya Mungu. Kama ninaweza kuiondoa dhamira ya kwanza njiani, Mungu ataitumia ile dhamira nyingine ikiwa Yeye ana jambo la kusema. Hiyo ni juu Yake.

196 Bali kama nikiweza kwa msaada wa Mungu. . .Ikiwa Yesu alikuwa amesimama hapa amevaa suti hii ambayo Yeye alinipa, kama wewe ni mgonjwa asingaliweza kukuponya; la, Yeye tayari amefanya hilo wakati alipokufa. Bali sijui kilichokuleta hapa. Wewe ni mwanamume tu. Tuko karibu, karibu rika moja, nasi tunaninii tu—tunasimama tu hapa mimbarani, tukikutana kwa mara ya kwanza. Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kunifunulia shauku zako, ama kile ulichofanya, ama vizuizi vyako? Kama Yeye anaweza kukuambia kile ambacho kimekuwako, anaweza kukuambia kitakachokuweko. Je! unaamini hilo?

197 Sitaki kuchukua muda mwingi kupita kiasi, bali nimehubiri kwa nguvu nanyi hamna budi kuninii. . .wakati, wasiwasi, inakubidi kupumzika kabisa, kwa sababu hakuna kitu niwezacho kufanya isipokuwa Yeye anionyeshe.

198 Naam, Hii hapa, Nuru ikija juu ya mtu huyu. Vema, bwana. Hapana, bwana, hupo hapa kwa ajili yako mwenyewe, upo hapa kwa ajili ya mtu mwingine, na huyo ni binti. Naye huyo binti anaishi California, na amekuwa na ajali ya motokaa, wakati fulani uliopita. Nawe unanitaka mimi. . .Umesimama, ili nimwombee huyo, maana angali anasumbuliwa na hiyo. Pia, sikiliza, hebu nikwambie jambo, ajali hiyo ya motokaa haikuwa California. Ilikuwa Dallas, Texas, ambapo ajali hiyo ya motokaa ilitukia. Je! hiyo ni kweli? Atakuwa mzima. Usisahau, ninamwona akitembea akiondoka. Vema, amini. Nenda na uamini sasa, ndugu. Mungu akubariki.

199 U hali gani, mama? Mimi ni mgeni kwako. Hatufahamiani mmoja na mwenzake. Hatufahamiani kabisa. Wewe ami-. . . unaamini Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Unamwamini Yeye? Sasa kama Roho Mtakatifu anaweza kuniambia jambo kukuhusu, ambalo unajua sijui, basi hilo litakufanya uamini, sivyo? Wewe ni. . .una matatizo. Una mambo mengi, lakini, lililo jambo lako kuu ni, uko karibu kukabili upasuaji kwa sababu ya kivimbe, na kivimbe hicho kiko ubavuni mwako. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hicho ndicho kimekuleta hapa kuombewa kwa ajili yake. Kama ningeweza kukuambia jina lako ni nani, ungeniamini mimi kuwa ni nabii Wake, au kuamini kwamba ingekuwa ni kweli? Bi Holman, nenda zako, ukifurahia. Unaona? Mungu akubariki. Amini sasa. Usitie shaka.

200 U hali gani, mama? Hatufahamiani mmoja kwa mwenzake. Wewe ni mdogo wa umri kuniliko, mwanamke tu na mwanamume.

201 Hebu kidogo, kila mtu awe na kicho kabisa. Roho wa Bwana aliondoka hapa.

202 Mtu huyu anayeketi *hapa*, amevaa miwani, una shida ya kiroho moyoni mwako. Hujui la kufanya. Umechanganyikiwa kabisa. Wewe amini, na utatoka vizuri. Naam, bwana. Je! utafanya hivyo? Vema.

Iweni na kicho sasa.

203 Huyu hapa maskini mama, ameketi papa hapa ndani, yeye akiangalia namna *hii*, na mikono yake, akiomba. Anao mkono mbaya anaoombea. Kama utaamini, naam, Mungu atauponya. Sikujui, hunijui, bali uligusa Kitu fulani. Kamwe hukunigusa mimi; uko futi ishirini kutoka kwangu. Yesu Kristo anakuponya. Imani yako inakufanya mzima.

204 Kama huyo siye Yesu yule yule, Kuhani Mkuu, awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu! Hivi hamwamini hilo kuwa ni hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

205 Samahani, lazima tu nifuate jinsi Hiyo inavyoenenda.

206 Ninakuwa dhaifu sasa, mnaona, ninii moja tu. . .Mwajua, Bwana wetu, mwanamke aligusa vazi Lake wakati mmoja na Yeye akasema. . .

207 Samahani, huyu mama mweusi anayeketi hapa, akiomba; shida ya kibofu nyongo, shinikizo kuu la damu. Amini, mama, litakuacha. Amina.

208 Niliangalia, kulikuwa na mama mweusi aliyesimama hapa, mnaona, imani yake ilivuta Hiyo moja kwa moja. Amina.

209 Huyo mama moja kwa moja nyuma yake, aliye na pumu. Kama utaamini kwamba Mungu atakuponya na hiyo pumu, waweza kuupata uponyaji, pia, kama utaamini.

210 Una shauku kubwa moyoni mwako, na hiyo ni sha—shauku halali. Unataka mtoto. Na sababu ya kutoweza kumpata, una tatizo la kike. Na hiyo ni kweli. [Dada huyo anasema, "Hiyo ndiyo niliyoandika kwenye kadi."—Mh.] Vema, je! unaamini sasa kwamba utakuwa. . .kwamba Mungu atakupa hiyo? ["Ndiyo. Hiyo ni kweli."] Ikiwa Bwana Yesu ataniambia kuwa wewe ni nani, je! utaamini? ["Ndiyo."] Bibi Lambert. ["Hiyo ni kweli."] Sasa wewe nenda, amini hiyo. Je! hiyo inakufanya uamini? ["Amina."] Jalia aipokee, Mungu, katika Jina la Yesu Kristo.

Kuwa na imani!

211 Bwana, hatufahamiani mmoja na mwenzake, bali Mungu anatujua sote wawili. Je! unaamini kwamba Bwana Yesu atanifunulia shida zako? Unaamini. Hutoki hapa. Hutoki Arizona. Unatoka mbali mashariki: Michigan. Hiyo ni kweli. Kweli. Una shinikizo kuu la damu, kukakamaa kwa ateri, ugumu wa kusikia. Imekuacha. Rudi Michigan, Bwana Yesu akuponya.

Mwamini Mungu!

212 Mama anayeketi hapa nje, akimwombea baba yake. Anao ugonjwa wa kutetemeka mwili. Na ninii. . .Ninamwona sasa, naye ametiwa uvuli. Sio tu kwamba ametiwa uvuli wa mauti, bali ni kifo cha Milele, kwa sababu hajaokoka. Hiyo ni kweli. Je! unaamini kwamba Mungu atamwokoa na kumponya? Kama una imani ya kutosha kumgusa Yesu Kristo, Kuhani wetu Mkuu, kwa kweli unaweza kukubali hiyo.

213 Sasa je! utanifanyia fadhili? Weka mkono wako juu ya mwanamke huyo aliye karibu nawe. Yeye anamwombea kaka yake. Naam. Huyo kaka ni mgonjwa, na pia ni mlevi wa pombe. Hiyo ni kweli. Amini tu, ataacha kunywa pombe na kuwa mzima.

"Ikiwa unaweza kuamini, yote yanawezekana!"

214 Mama huyu anayeketi hapa, akiomba, papa hapa mbele yangu, ameinamisha kichwa chake. Ninaweza kukuambia, yeye anaomba, "Bwana, jalia iwe ni mimi." Mama huyo ni. . . Anamwombea rafiki, naye rafiki huyo yupo hapa hospitalini, akifa kwa kansa; na kwa ajili yake mwenyewe, pia. Ataikosa. Bibi Kelly, simama kwa miguu yako na upokee uponyaji, katika Jina la Yesu Kristo. Sijawahi kumwona mwanamke huyo, maishani mwangu.

215 Je! unaamini kwamba Mungu huponya ugonjwa wa moyo? Je! unaamini kwamba anaponya wako? Vema, basi endelea tu kusonga, ukisema, "Asante, Mungu Mpendwa."

216 Ni vigumu kwako kuamka asubuhi, umekakamaa sana na hiyo baridi yabisi. Haitakuwa hivyo kesho ikiwa tu utaamini na kuendelea. Naam, bwana.

217 Vema, bwana. Unahitaji kuongezwa damu kutoka Kalvari, inaponya kisukari na kila kitu. Unaamini kwamba Yeye hufanya

hivyo? Vema, chako chaweza kuponywa, pia, ikiwa tu utaamini kwa moyo wako wote.

218 Njoo hapa. Una wasiwasi, hilo ndilo limesababisha matatizo yako. Una tumbo lenye vidonda. Je! unaamini kwamba Mungu ataliponya? [Dada huyo asema, "Ndiyo, ninaamini."—Mh.] Ninataka kukuonyesha jambo fulani. Nitaivua saa yangu ya mkono kwa dakika moja tu. Wasiwasi, kwa namna fulani ni vigumu, lakini wewe ni mtu mwema. Hebu nishike mkono wako. Ninataka kushika mkono wako. Ninataka uangalie mkono wangu. Sasa angalia, ukienda kuweka mkono wako juu ya wangu. Sasa unaiona, unaviona vitu hivyo vikikimbia pale, vitu kama mitetemo midogo? ["Ndiyo, ninaona."] Hivyo ni vidonda vilivyo hai. Sasa angalia, toa mkono wako, sasa unarudi kuwa kawaida. Sasa nitaweka mkono wangu juu hapo, haifanyi hivyo, sivyo? ["La."] Bali nitaweka mkono wako juu yake, hiyo hapo tena. Unaona? ["Ndiyo."] Sasa kuna kitu fulani kinaashiria pale, ambacho kwa kweli unaweza kuona kwa macho yako mwenyewe. Je! hiyo ni kweli? ["Ndiyo. Amina."] Inua mkono wako ili kusanyiko liweze kuona kuwa hiyo ni kweli.

219 *Hapa*, kusanyiko linaweza kuiona. Weka mkono wako hapa juu. Sasa toa mkono wako, mama. Sasa weka mkono wako hapo tena. Ni kidonda hai. Ni msuli, kitu fulani kinakula msuli. Inatokana na wasiwasi, inaenea. Una tatizo la kina mama, pia. Vema.

220 Sasa, hapa, huu ndio wakati inapokubidi kuchukua hatua, kusudi tu huyu mama ajue.

221 Sasa ninataka kusanyiko kuendelea kuinamisha vichwa vyao, na kuomba, maana inaenda kutoka kwa mmoja hadi mwingine. Wakati inapokulazimu ku. . . Yesu alisema, "Katika Jina Langu watatoa pepo." Sasa wewe endelea kuinamisha kichwa chako kama hutaki kidonda. Unaona?

222 Sasa hapa nataka uangalie. Unacho kidonda, sasa wewe angalia mkono wangu na uone kwamba sisogezi mkono wangu.

223 Baba wa Mbinguni, naomba rehema Zako na neema ziwe juu ya mwanamke huyu, kumpa afya. Yeye anauangalia mkono wangu. Anaangalia, Baba, kuona kama kuna badiliko lolote. Nami najua kwamba, imani yake, akiwa na wasiwasi, ninaomba, Mungu, kwamba Wewe utamsaidia. Katika Jina la Yesu, msaidie.

224 Sasa, huyo mama, sijafungua macho yangu bado, bali mama huyo anajua kwamba mkono wangu ungali unabaki jinsi ulivyokuwa. Hiyo si ni kweli, mama? [Dada anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] Sasa angalia kwa makini sasa.

225 Kwa hiyo, hili halifanywi ili kufanya maonyesho. Hili linafanywa kutangaza kwamba Yesu hutimiza Neno Lake. Sasa, Yeye alisema, "Katika Jina Langu watatoa pepo."

226 Sasa ninaenda kushikilia mkono wangu imara kabisa. Nami ninataka uone, si vile ninavyoshikilia mkono wangu. Unaona, upo hapo wakati wote. Unaona jinsi unavyovimba? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Unakuwa mbaya zaidi kila wakati ["Ndiyo."] maana ninashikilia. Mkono wangu wote umekufa ganzi, hadi kwenye kiwiko changu. Sasa wewe uangalie tu kwa muda kidogo.

227 Bwana Yesu, si kwa maonyesho (hatupaswi kufanya hivyo), bali ili Neno Lako litimizwe. Wewe hukuwaponya watu ili tu kuonyesha Wewe ulikuwa ni Mungu, bali ilikuwa ni kutimiza Neno. Na hivyo ndivyo mimi. . . sababu ya mimi kufanya hili usiku wa leo, Baba, ni imani yangu kuamini kwamba mwanamke huyu mzuri anaweza kuponywa kutokana na pepo huyu.

228 Shetani, nakuapisha, katika Jina la Yesu Kristo, Yeye aliyeshinda magonjwa yote, na yako chini ya miguu Yake. Na kama mtumishi Wake, ninachukua hatua. Katika Jina la Yesu, mwache mwanamke huyu, toka ndani yake.

229 Sasa sijausogeza mkono wangu. Mama huyo akiwa ni shahidi wangu. Kitu fulani kilifanyikia mkono wangu, sivyo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] Kama hiyo ni kweli, sema, "Amina." ["Ndiyo. Amina."] Imekwisha, sivyo? ["Ndiyo. Amina. Imekwisha."] Umeponywa. ["Haleluya!"] Sasa huyo hapo. ["Asante, Yesu!"] Sasa angalia hapa. Ninaweka mkono wangu juu yake, sasa weka mkono wako juu yake, ni sawa tu. ["Ndiyo. Amina."] Umeponywa. ["Ndiyo. Amina. Haleluya!"] Endelea, nenda ukale chakula chako cha jioni, Yesu Kristo anakuponya.

"Katika Jina Langu watatoa pepo!" Naam.

230 Je! unaamini, dada? Je! unaamini? Unaamini kwamba Mungu anaweza kukuondolea ugonjwa huo wa pumu na akupe afya? Vema, nenda zako, useme, "Asante, Bwana Yesu. Ninakuamini Wewe, kwa moyo wangu wote."

231 U hali gani, bwana? Moyo umekuwa ukikusumbua, namna fulani ya kuzibika kulikoletwa na wasiwasi; midundo, mdundo maradufu, mmoja kwenye. . . miwili upande mmoja, na mmoja upande mwingine. Vema, bwana, inakoma sasa. Endelea. Imani yako inakuponya, bwana. Nenda, ukiamini kwa moyo wako wote. Vema.

232 Tumbo lingine, baya. Je! unaamini kwamba Yesu anakuponya? Nenda tu, useme, "Asante, Bwana Yesu." Amini. Kama Yeye anaweza kukuambia kile ulicho, hakika anaweza kukuponya.

233 Vipi kama sikukuambia neno moja, nikuwekee tu mikono, je! ungeamini kwamba uliponywa, unayeketi hapo kitini? Ungeamini? Nenda zako, useme, "Asante, Bwana." Ni kile unachoamini.

234 Njoo. Je! unaamini ya kwamba Mungu aliuponya ugonjwa huo wa mgongo, ukiwa umeketi hapo basi? Vema, unaweza kuendelea, useme, “Asante, Bwana.” Amini kwa moyo wako wote. Endelea na uamini.

235 Bwana, Mungu asipokuponya, siku moja utalemaa, namna *hii*, ukiwa na fimbo, ukitembea na hiyo baridi yabisi. Kwa nini usimkubali sasa hivi? Je! unaamini? Nenda zako, na useme, “Asante, Bwana.” Na ukanyage kitu hicho, na uende zako, ukifurahia.

236 Yesu anaponya mgongo wako na kukupa afya. Unaamini hilo? Vema, nenda zako, ukisema, “Asante, Mungu Mpendwa.”

237 Njoo hapa, mama. Sasa unaogopa nini? Sababu ya wewe kuogopa, ni wakati wako wa kukoma hedhi. Unajua ninachomaanisha, badiliko la mwanamke. Na kila kitu, wakati wa jioni sana, unakuwa mchovu. Huwezi kufanya kazi yako, unachoka sana. Hiyo si ni kweli? [Dada huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Vema. Ni sawa sasa. Endelea, imani yako inakuponya.

238 Mwingine, wasiwasi, bali umekuwa na wasiwasi maisha yako yote, umekuwa na wasiwasi kidogo ulipokuwa mdogo zaidi. Ulikuwa ni maskini mwoga ukizunguka. Lakini sasa inaonekana kana kwamba kitu fulani kimekushika. Umesongwa kila wakati. Hiyo si ni kweli? Haitakuweko tena, kama utaniamini sasa kama nabii wa Mungu. Nenda na uamini.

239 Ni wangapi huko nje mnaoamini kwa mioyo yenu yote? Wekeaneni mikono nyinyi kwa nyinyi. Katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ninamwagiza kila mwanamume na mwanamke hapa kuweka mikono yenu mmoja juu ya mwenzake.

240 Ikiwa Neno la Mungu, sehemu Yake ni kweli, Yote ni kweli. Yesu Kristo alisema, “Katika—katika Jina Langu watatoa pepo.” “Neno la Mungu ni Tambuzi la mawazo na makusudi ya moyo.”

241 Yesu alisema, “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Kila mwaminio humu ndani, sema “amina” kwa hilo. [Kusanyiko linasema “Amina.”—Mh.] Basi, nyinyi ni waaminio, wewe mwombee yule aliye na . . . Wewe mwombee yule aliyekuwekea mkono wake, kwa kuwa wao wanakuombea. Hebu tuombe pamoja na kumshinda adui, na hebu kila mtu mgonjwa humu ndani aponywe, katika Uwepo wa Yesu Kristo.

242 Mungu Mwenyezi, Mwanzilishi wa Uhai, Mpaji wa karama zote nzuri, zitume baraka Zako juu ya watu hawa.

243 Shetani, umeshindwa vita. Yesu Kristo yupo hapa. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Wakristo wamewekeana mikono. Wanaomba maombi ya imani.

244 Wewe ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Kila mmoja wao alisema, “Amina,” wanaamini. Walitafsiri

shauku ya moyo Wako, wakati Wewe uliposema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Wamewekeana mikono.

245 Umeshindwa, ewe Shetani. Toka ndani yao, katika Jina la Yesu Kristo. Toka mahali hapa na uondoke kwenye jengo hili, katika Jina la Yesu Kristo.

246 Kila mwanamume na mwanamke anayeamini kwamba mwaminio amekuwekea mikono, maombi ya imani yameombwa, nawe uko tayari kuuacha ugonjwa wako, uyaache mawazo yako kuuhusu, na kulikubali Neno la Mungu kuingia moyoni mwako, simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina na amina! Inueni mikono yenu sasa na kumpa sifa, kwa kuwa yote yamekwisha.

*Kumtazama Yesu* SWA64-0122
(Looking Unto Jesus)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 22 Januari, 1964, katika Hoteli ya Ramada kule Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani  kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org